# Nipashe

Jumamosi Desemba 28, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581904

www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US Nipashe digital

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com




UKURASA WA 3

**Gwajima** ataka wazazi kuimarisha ulinzi kwa Watoto

UKURASA WA 5

**Mwinyi** ahimiza kauli maridhawa kuepusha jamii na mifarakano

UKURASA WA 16

TULIKOTOKA

**Kasongo** mbona wewo, wimbo wa mwaka 1980, 'unaotrendi' kama utani mwaka 2024



## SALAH: UBINGWA EPL MSIMU HUU NI WETU

UKURASA 21

# Taharuki yatanda kwa meli kutitia bandarini

UKURASA 2




Meli ya MV Serengeti ikiwa imetitia ndani ya maji upande wa nyuma katika bandari ya Mwanza Kusini ilipoegeshwa kusubiri matengenezo, kulia ni chelezo kinachozamishwa kwa ajili ya kuinua meli hiyo. Chanzo cha kutitia kwa meli hiyo ambayo ni ya pili kwa mwaka huu kuzama ikiwa imeegeshwa bandarini bado kinachunguzwa. **PICHA: VITUS AUDAX**

UKURASA WA 4

## ASKOFU MWAMAKULA ATAJA MAMBO SITA KWA SERIKALI KUYAFANYIA KAZI

## Miili watu sita yatambuliwa ajali ya Rombo

UKURASA 3



# Askofu Anglikana anusurika katika ajali

UKURASA 2

**MICHEZO** **MABONDIA WAZAWA KATIKA TKO YA RAIS SAMIA** UK.23

**MAONI,** UK.6

# Askofu Anglikana anusurika katika ajali

**Na Jenifer Gilla**

ASKOFU wa Kanisa Anglikana Dayosisi ya Zanzibar, Michael Hafidh, amenusurika katika ajali mbaya iliyotokea juzi Handeni, Tanga ikihusisha basi la abiria na lori na kuua watu 11 na wengine 13 kujeruhiwa.

Ajali hiyo ilitokea juzi saa 3:00 usiku baada ya lori aina ya Mistubishi Fuso lililokuwa likitolea Lushoto kwenda Dar es Salaam kugongana na basi dogo aina ya Toyota Coaster lililokuwa likitokea Mkata, wilayani handeni, kwenda jijini Tanga.

Mmoja kati ya viongozi wa juu wa Kanisa Anglikana Tanzania, Makao makuu Dodoma, ambaye hakutaka jina lake liandikwe, alithibitisha Askofu Hafidh kupata ajali hiyo kisha kupelekwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa matibabu na sasa anaendelea vizuri.

Juzi, Umoja wa Anglikana wa Kueneza Injili kupitia mtandao wa kijamii wa 'facebook' ulieleza kuwa Askofu Hafidh alipata ajali akiwa katika basi la abiria liligongana na lori na kujeruhiwa kisha kupelekwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) pamoja na majeruhi wengine.

Taarifa hiyo ilisema kutokana na hali hiyo Askofu wa Kanisa Anglikana Dayosisi ya Dar es Salaam, Jackson Sosthenes, na viongozi wengine wa dini walikwenda kumtembelea na kumjulia hali.

Aidha, taarifa hiyo ilisema Askofu Hafidh alipotembelewa na viongozi hao, alimtambua Askofu Sosthenes, hali iliyoonesha kuwa kuna unafuu wa afya yake tofauti na alipokuwa amefikishwa hospitalini hapo.

Hata hivyo, taarifa ambazo gazeti hili lilizipata na kuthibitishwa na Ofisa Uhusiano kwa Umma wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Abdallah Nassoro, zilieleza kuwa Askofu Hafidh, anaendelea na matibabu katika taasisi hiyo baada ya kuhamishiwa kutoka MNH.

"Ni kweli Askofu yupo hapa MOI anaendelea na matibabu baada ya kuhamishiwa kutokea Muhimbili. Ninachoweza kusema ni kwamba yuko hapa anaendelea na matibabu," alisema Nassoro.

**KAULI ASKOFU MKUU**

Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dk. Maimbo Mndolwa, aliwaeleza waumini wa kanisa hilo kuwa hali ya afya ya Askofu Hafidh, inaendelea kuimarika.

Askofu Dk. Mndolwa alitoa kauli hiyo jana kwenye Ibada ya Misa Takatifu ya Shukrani ya Familia ya Askofu Mkuu iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Patrick Bagamoyo, Dinari ya Vugiri, Korogwe.

Alisema Askofu Hafidh alikuwa miongoni mwa wasafiri waliopata ajali ya gari iliyotokea mapema juzi katika eneo la Kwenkwale, kata ya Kitumbi, Handeni mkoani Tanga.

"Tumepokea taarifa za ajali ambayo imesababisha vifo vya baadhi ya wasafiri na majeruhi akiwamo Askofu Hafidh ambaye licha ya majeraha aliyoyapata, tunamshukuru Mungu alitoka salama na anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili," alisema .

Askofu Dk. Mndolwa alisema kanisa linatoa salamu za pole kwa familia zilizopoteza wapendwa wao katika ajali hiyo na kuwaombea majeruhi wapone haraka ili warudi kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa.

**ASKOFU MWAMAKULA**

Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania na Afrika Mashariki, Emmaus Mwamakula, katika ukurasa wake wa facebook, alieleza kusikitishwa na taarifa hiyo na na kuliomba Kanisa la Tanzania kumuombea Askofu Hafidh pamoja na majeruhi wote ili Mungu awafanyie wepesi na kuwaponya.

Juzi, Mkuu wa Wilaya ya Handeni , Wakili Albert Msando, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuwa majeruhi 13 walipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni kwa ajili ya kupata matibabu.

"Watu 11 walifariki dunia wakiwamo madereva wa magari yote mawili na majeruhi 13 wamepelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Handeni kwa ajili ya kupata matibabu. Kati yao majeruhi tisa hali zao si nzuri na madaktari wanaendelea na juhudi za matibabu,.

"Tuendelee kuwaombea familia za watu wote waliofariki katika ajali hiyo. Mungu akawakumbuke marehemu waliofariki. Raha ya milele uwape, Ee Bwana. Mwanga wa milele uwaangazie. Wapumzike kwa amani," alisema.



Viongozi wa Kanisa la Glory Temple lililopo kata ya Maweni (Kange Juu) jijini Tanga, wakitoa zawadi na misaada kwa makundi mbalimbali yenye mahitaji maalumu ikiwemo wazee, walemavu, wajane na waraibu wa dawa za kulevya juzi ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Taharuki yatanda meli kutitia bandarini

**Na Vitus Audax,** MWANZA

TAHARUKI ilitanda kwa wakazi wa Mwanza baada ya kuwapo taarifa kuwa meli ya MV. Serengeti, imetitia upande wa nyuma na kuzama ziwani ikiwa imeegeshwa katika bandari ya Mwanza South.

Tukio hilo limetokea zikiwa zimepita siku 222 baada ya meli ya MV. Clarias kupinduka na kuanguka majini ikiwa imeegeshwa katika bandari ya Mwanza North. Taarifa za kutitia kwa meli hiyo yenye uwezo wa kubeba abiria 500 na tani 250 za mizigo, zilienea juzi katika mitandao ya kijamii kwamba imezama ikiwa na mizigo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii eneo la bandari hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO), Wakili Alphonce Sebukoto, alikiri kutitia kwa meli na kusema haikuwa na safari yoyote tangu mwaka 2016.

Sebukoto alisema walipata taarifa kutoka kwa walinzi wa eneo hilo juu ya meli hiyo kutitia na sehemu ya nyuma kuanza kuzama usiku wa kuamkia Desemba 26, majira ya saa 7:00 usiku, hivyo kutuma wataalamu kuanza juhudi za kuiinua.

Alisema meli hiyo ni miongoni mwa meli nne ambazo haziko kwenye uendeshwaji na zimeegeshwa katika bandari hiyo inayotumika kuegesha meli ambazo zinasubiri matengenezo.

"Si kweli kwamba meli hii ilikuwa na mizigo bali tangu mwaka 2016 imeegeshwa kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo makubwa. Kilichotokea ni maji kuingia ndani ya meli kwa nyuma na kuanza kuzama majini, hivyo wataalam wetu kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji upande wa majini, wanaendelea na jitihada za kuiondoa ili uchunguzi wa chanzo uanze,"alisema Wakili Sebukoto.

Pia alisema baada ya kuinuliwa itapandishwa kwenye chelezo ambako watachunguza kujua sababu ya maji kuingia ndani ya meli hiyo ambayo imetengenezwa mwaka 1988 na imekaa bandarini hapo kwa miaka tisa.

**UCHUNGUZI MV.CLARIAS**

Kuhusu uchunguzi uliotangazwa kuanza kufanyika tangu Mei, mwaka huu, ilipozama meli ya MV. Clarias muda mfupi baada ya kutoka kwenye safari zake, Sebukoto alisema matukio hayo yana tofauti.

Alisema kutokana na kuwa meli hiyo haikuwa na tatizo lolote na ilikuwa inaendelea na safari, uchunguzi unaendelea kupitia kamati ya ulinzi na usalama ili kubaini kama ajali hiyo ilitokea bahati mbaya au makusudi.

"Ilibainika kuwa matundu maalum ya kuruhusu meli kupumua 'stern tube' yalikutwa na upana usio wa kawaida hali iliyoruhusu maji kuingia kwa wingi na kusababisha uzito kuegemea upande mmoja. Tatizo hilo linaweza kusababishwa na ama maji kuingia au kushushwa kwa mkono wa binadamu," alisema Sebukoto. Pia alisema taarifa kuhusu jambo hilo zitatolewa mara baada ya uchunguzi na ikibainika kuna uzembe au hujuma uliyofanyika wahusika watafikishwa mahakamani kwa kuwa serikali haiwezi kuvumilia kuona vyombo vyake vikihujumiwa.

Katika kuhakikisha matukio hayo hayajirudii, alisema TASHICO ina mpango wa kuweka mifumo ya kiusalama ya kidijitali zikiwamo kamera ili pale linapokaribia kutokea tukio la namna hiyo, lidhibitiwe mapema.

"Hizi meli zetu zimetengenezwa katika mifumo ya zamani, hivyo hazina 'alarm' ambazo zinasaidia kutambua tatizo endapo maji au moshi usiohitajika ukiingia. Pia hazina kamera, hivyo mpango ni kufunga vitu hivyo ili kutoa taarifa mapema," alisema.

Akizungumza wakati wa uokoaji wa meli hiyo, Kiongozi wa Kitengo cha Uokoaji Ndani ya Maji kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Mkaguzi Msaidizi Said Sekibojo, alisema hakuna madhara yaliyopatikana kwenye chombo hicho na taratibu za kukitoa majini zinaendelea.

"Kazi kubwa tunayoifanya ni kuifunga na kuanza kuinyanyua, kisha kumwaga maji ambako tunaendelea hatua hiyo na kufikia leo (jana) jioni tunatarajia kuwa tumekamilisha kila kitu," alisema Sekibojo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



## ACT yaomba uteuzi wa waziri utenguliwe

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo Visiwani Zanzibar kimemuomba Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, atengue uteuzi wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, kwa madai kwamba ameshindwa kusimamia ipasavyo idara hizo maalum za SMZ.

Kadhalika, kimemwomba Rais Mwinyi aunde tume huru ya kijaji kuchunguza mauaji yote yaliyotokea hivi karibuni visiwani Zanzibar.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Msemaji, Kamati ya Wasemaji wa Kisekta wa chama hicho Zanzibar, Hamad Mussa Yussuf, chama hicho kimedai kutokea kwa vifo vya utata kwa watu wawili na mmoja akiwa hajulikani alipo.

"Chama cha ACT- Wazalendo, tumepokea kwa masikitiko na huzuni kubwa taarifa ya kuuliwa kwa watu wawili na mtu mmoja ambaye haijulikani alipo mpaka sasa, tukio lililotokea katika kijiji cha Kiungoni, jimbo la Pandani wilaya ya Wete mkoa wa Kaskazini Pemba.

"Waliouawa ni Athumani Hamad Athumani na Amour Khamisi Salim, mtu mwingine wa tatu ambaye hajulikani alipo ni Mbarouk Abdalla Khamis. Watu hawa walichukuliwa usiku wa kuamkia Desemba 24 mwaka huu wakiwa wazima wa afya.

"Desemba 24 saa 1:30 usiku, maiti za watu wawili zilipelekwa kwa familia zao kwa ajili ya taratibu za mazishi bila ya maelezo yoyote yale,"alisema Yusuf.

Msemaji huyo wa ACT-Wazalendo Zanzibar, alidai kwamba tukio hilo linafanana na la mauaji lililowahi kutokea hivi karibuni katika eneo la Kidoti, mkoa wa Kaskazini Unguja.

"Matukio haya yanazidi kudhoofisha na kutia wasiwasi kuhusu usalama wa maisha na amani ya wananchi Zanzibar,"alisema Yusuf.

Alilitaka Jeshi la Polisi Zanzibar, kuhakikisha kwamba linatimiza wajibu wake wa kulinda raia na mali zao kwa kuwahakikishia usalama wao, raia wanaoishi humo kutokuwa na hofu ya maisha yao.

Kadhalika, alilitaka Jeshi hilo, kuwakamata wote waliohusika na mauaji hayo pamoja na mengine yaliyotokea hivi karibuni ikiwamo kuwafikisha mahakamani waliohusika na matukio hayo.

Pia, alilitaka Jeshi hilo, kuweka wazi ripoti ya Tume ya kuchunguza mauaji yaliyotokea Novemba 9 mwaka huu katika eneo la Kidoti visiwani humo.

# Miili sita yatambuliwa ajali ya Kibaoni

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

WAKATI idadi ya watu walipoteza maisha katika ajali ya barabarani iliyotokea Kijiji cha Kibaoni-Tarakea, Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro ikifikia 10, hadi sasa waliotambuliwa ni watu sita pekee.

Ajali hiyo iliyotokea barabara kuu ya Moshi/Tarakea, majira ya saa 9:40 jioni ya Desemba 26, mwaka huu, ilihusisha basi la abiria, mali ya Kampuni ya Ngasere, lenye namba za usajili T 620 DZQ lililokuwa likitokea Dodoma kwenda Tarakea, kugongana uso kwa uso na gari dogo la abiria aina ya Toyota Noah, namba T 959 CKU, lililokuwa likitokea Tarakea kwenda Moshi.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Simon Maigwa, mpaka sasa waliotambuliwa ni watu sita kati ya 10 waliokuwamo ndani ya Noah.

Aliwataja waliotambuliwa kuwa ni Mamasita Lowassa (27), mkazi wa Kamwanga ambaye alikuwa dereva wa Noah na Damarisi Mwikau (22), mkazi wa Elast, nchini Kenya.

Wengine ni Peter Urio (38), Monica Mumbua, raia wa Kenya, Eligatanasi Kanje (30), mkazi wa Tarakea na Hilda Liberatus (24), mkazi wa Kikelelwa, huku polisi ikieleza miili ambayo bado haijatambuliwa ni minne.

Aidha, Kamanda Maigwa ametaja chanzo cha ajali hiyo, ni uzembe wa dereva wa gari dogo la abiria aina ya Noah kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari.

Jana katika ukurasa wake wa mitandao ya kijamii, Rais Samia Suluhu Hassan alisema: "Nimesikitishwa na taarifa ya vifo vya ndugu zetu tisa kutokana na ajali ya barabarani iliyotokea katika barabara ya kutoka Tarekea, Wilaya ya Rombo kuelekea mji wa Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro.

"Ninawaombea marehemu wapumzike kwa amani. Ninatoa salamu za pole kwa wafiwa, ndugu na jamaa na ninawaombea majeruhi wapate nafuu kwa haraka.

...Nasisitiza madereva kuendelea kuwa makini na waangalifu zaidi barabarani, huku Jeshi la Polisi likiendelea na kazi ya kusimamia sheria za usalama barabarani wakati huu wa mwisho wa mwaka."



Mwandikishaji wa uboreshaji wa daftari la kudumu la Mpiga kura Winfrida Kihanga akimwandisha Mpiga kura wa Kituo Cha Mkimbizi D mjini Iringa Ayub Fungo kwenye daftari la kudumu la Mpiga kura zoezi la uboreshaji wa taarifa za wapiga kura limeanza Jana Disemba 12-2Jan 2025. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Gwajima ataka wazazi kuimarisha ulinzi kwa watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wazazi na walezi kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto kutokana na utafiti kuonesha ndugu na jamaa wa karibu ndio wanaongoza kuwafanyia ukatili.

Dk. Gwajima, alibainisha hayo juzi kwenye taarifa yake iliyotolewa kwa umma kulaani tukio la mauaji ya mtoto Grayson Kanyenye (6), anayedaiwa kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito katika eneo la Ilazo, jijini hapa.

Mtoto huyo anadaiwa kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani wakati mama yake akiwa ametoka kwenda kutembea usiku wa kuamkia Sikukuu ya Krismasi na kumwacha kwa dereva wa bodaboda.

Katika taarifa yake Dk. Gwajima alisema wizara imepokea taarifa hizo za masikitiko kwa simanzi kubwa kutokana na mtoto huyo kukatishwa uhai wakati alikua anaanza safari ya ndoto yake.

"Natoa pole nyingi kwa wazazi wa mtoto ndugu na jamaa kwa msiba huu mkubwa uliogusa hisia za wengi, natoa wito kwa wazazi na walezi kuimarisha ulinzi na usalama wa watoto na kukumbuka kuwa tafiti zinaonesha ndugu na jamaa wa karibu ndiyo wanaongoza kuwafanyia watoto ukatili ikiwa ni pamoja na ubakaji, ulawiti na hata mauaji," alisema Dk. Gwajima.

Aidha, alisema ni imani yake kuwa vyombo vya kusimamia sheria vitafuatilia jambo hilo kwa kadri iwezekanavyo ili wahusika wabainike na haki ya mtoto ipatikane na kuwa funzo kwa wengine wanaofanya ukatili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, George Katabazi, akizungumzia tukio hilo juzi, alisema mwili wa mtoto huyo ulikutwa ndani ya nyumba ukiwa na majeraha shingoni.

Katabazi, alisema tukio litokea majira ya saa 1:00 asubuhi katika Mtaa wa Bwawani, Ilazo Extension jijini Dodoma, nyumbani kwa Ofisa Uvuvi wa Mtera, Hamis Mohamed.

Alisema, Hamis na mama wa mtoto huyo walitoka kwenda matembezini na kumwacha chini ya usimamizi wa dereva bodaboda maeneo ya Ilazo Extension jijini hapa, Kelvin Gilbert.

Alisema, inadaiwa kuwa bodaboda huyo walimfahamu kupitia huduma ya usafiri anayoitoa kwa familia hiyo.

"Bodaboda huyu aliachiwa mtoto ili amwangalie kipindi ambacho watakuwa kwenye matembezi wawili hao wakati wa usiku, lakini waliporudi mtoto hawakumuona hadi asubuhi majira ya saa 1:00 walipomkuta kwenye chumba akiwa ameuawa na alama za kupigwa na kitu kizito shingoni mwake," alisema.

Kadhalika, Kamanda Katabazi alisema Jeshi la Polisi mkoani hapa linamshikilia bodaboda huyo kwa ajili ya uchunguzi zaidi wa tukio hilo la mauaji.

"Tumemkamata bodaboda huyo kwa ajili ya uchunguzi wa tukio hili ambapo yeye amekanusha kuhusika na jambo hili, lakini tunaendelea na uchunguzi ili kubaini nini hasa kilitokea kwa mtoto huyu na kupelekea kifo chake," alisema Katabazi.

Aidha, Kamanda alitoa wito kwa wazazi kuacha tabia ya kukabidhi watoto wao kwa watu ambao hawawajui vizuri ili kuepusha matukio kama hayo.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Othman asisitiza weledi utoaji haki

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka watendaji wa mahakama Zanzibar kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kwenda sambamba na uwekezaji mkubwa wa fedha unaofanywa na serikali hasa katika suala la miundombinu na majengo ya kisasa.

Taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Habari Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ilisema Othman aliyasema hayo jana Kinyasini wilaya ya Wete, mkoa wa Kaskazini Pemba alipoweka jiwe la msingi la jengo jipya la kisasa la Mahakama ya Mkoa Pemba linalojengwa ikiwa ni sehemu ya mkakati wa serikali kuimarisha huduma za utoaji haki kupitia mahakama.

Alisema ni vyema watendaji wa mahakama wakaimarisha huduma na upatikanaji wa haki kwa wananchi ili mahakama iwe kimbilio lao badala ya kuikimbia kutokana na kukosa imani na mhimili huo.

Othman alisema mahakama pia zinapaswa kuwa chombo cha kuchunguza matukio ya vifo vya ghafla na mengine ya namna hiyo kwa kuunda tume zenye usimamizi wa majaji wanaoaminika na jamii.

Alisema kufanya hivyo kutajenga imani kubwa kwa wananchi na chombo hicho pia kutimiza malengo ya serikali ya kuimarishia miundombinu yakiwamo majengo ya ofisi za majaji, mahakimu, makadhi na watendaji wengine kwenye kada hiyo muhimu katika upatikanaji wa haki.

Jaji Mkuu wa Zanzibar, kwa mujibu wa Othman, ana uwezo na wajibu wa kisheria kusimamia uchunguzi wa kesi na matukio ya mauaji mbalimbali chini ya utaratibu wa kuunda tume itakayosimamiwa na jaji anayeaminika ndani ya jamii

Adha, Othman aliwaeleza watendaji hao kwamba hadhi ya chombo hicho haitakuwapo kwa kuwa na majengo mazuri yaliyojengwa kwa gharama kubwa pekee bali itatokana na namna mahakama katika ngazi mbalimbali zinavyosimamia mashauri na haki kupatikana.

Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan, alisema hivi sasa mahakama mbalimbali zimeimairisha na kuharakisha kusikiliza mashauri mbalimbali na kumaliza kesi nyingi kwa wakati. Hatua hiyo, alisema imefanikisha kumaliza mrundikano wa kesi.

Alisema chombo hicho pia kimepata mkopo wa dola milioni 30 ambazo zitatumika katika uimarishaji wa mahakama awamu inayofuata na kukifanya kuwa na utendaji wa kisasa ulioimarika kwa vifaa na miundombinu ya kisasa pamoja na watendaji mahiri wenye utaalamu bora.

Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria, Shamata Shaame Khamis, alisema ujenzi wa majengo ya mahakama ni sehemu ya kuendeleza maboresho muhimu katika chombo hicho kupitia bajeti inayotengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuwapatia wananchi huduma bora.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema mkoa huo katika kipindi cha kuelekea kilele cha miaka 61 ya Mapinduzi, miradi 18 itazinduliwa na mingine kuwekewa mawe ya msingi na baadhi kufunguliwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana katika uendelezaji wa miradi ya maendeleo na kwamba kwa upande wa mahakama hivi sasa inashuhudiwa kuwapo mabadiliko makubwa ya kuboresha miundombinu ikiwamo ujenzi wa ofisi za kisasa.

Hafla hiyo ilikuwa sehemu ya shughuli mbalimbali zinazoendelea hivi sasa Unguja na Pemba za shamrashamra za kutimiza miaka 61 ya Mapinduzi Zanzibar ya Januari 1964 na kilele cha sherehe hizo kitafanyika Januari 12, 2025.



Mwendesha pikipiki akipita kwa tabu kwenye barabara yenye tope Mvuti Mianzini wilaya ya Ilala baada ya kunyesha mvua ambayo ilisababisha utelezi kwa vyombo vya moto hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Askofu Mwamakula ataja mambo sita kwa serikali kuyafanyia kazi

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania na Afrika Mashariki, Emmaus Mwamakula, ametoa ujumbe mzito akiitaka serikali kushughulikia changamoto sita zinazoikabili jamii ili washerehekee sikukuu ya Krismasi wakiwa na amani mioyoni mwao.

Alizitaja changamoto hizo kuwa ni usalama wa maisha ya watu na mali zao, ukosefu wa ajira, uhalifu wa kisiasa, gharama za maisha, gharama za matibabu na ubora wa elimu.

Alisema mambo hayo yanabeba msingi wa haki ambayo kama ikitoweka katika jamii ni vigumu Watanzania kuendelea kuimba wimbo wa gloria na unaoitangaza amani wakati mioyo yao imejaa simanzi.

Alisema msingi mkuu wa ujumbe wa wimbo wa Krismasi wa Gloria (utukufu) na pax (amani) umetikiswa na matumaini ya watu wengi yametoweka, hivyo ni jukumu la wananchi kuomba, kusema na kutenda na walio katika nafasi na mamlaka kujihoji na kuchukua hatua kuhusiana na changamoto zilizoelezwa.

Kwa mujibu wa Askofu Mwamakula, usalama kwa maisha ya watu na mali zao umezorota kwa kiasi kikubwa, ukichochewa na vitendo vya utekaji na mauaji vilivyoikumba jamii katika taharuki ikishuhudia watu kadhaa wakiuawa na watu wasiojulikana na wengine kutekwa miezi sita iliyopita.

Alisema pia hali ya usalama wa majengo inaogopesha kwani jamii imeshuhudia baadhi yake yakiungua moto na mengine kuporomoka na kusababisha vifo na majeruhi kutokana na uwezo wa uokozi kuwa mdogo.

> **" Bidhaa bandia zinatishia hali ya afya huku kukiwa na hofu ya uwepo wa bidhaa zilizoisha muda wake madukani, " alisema**

" Bidhaa bandia zinatishia hali ya afya huku kukiwa na hofu ya uwepo wa bidhaa zilizoisha muda wake madukani, " alisema

Alisema ukosefu wa ajira umesababisha vijana wengi waliohitimu katika shule, vyuo vikuu kujiingiza katika uhalifu wa aina mbalimbali ikiwamo wa mtandaoni na wale waliofuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) bila kupatiwa ajira wanatumiwa na watu wenye nguvu, pesa, mali na mamlaka katika vitendo vya utekaji.

Hali hiyo, alisema huchochea baadhi ya vijana kuingia katika mitego ya kurubuniwa kwa fedha kidogo na kutumika katika vikosi vya ugaidi duniani hasa katika nchi jirani.

Kwa mujibu wa Mwamakula uhalifu wa kisiasa unaonekana ukihalalishwa na watu wenye mamlaka kiasi cha kupelekea hata kufanyika kwa mauaji wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba, mwaka huu. Mambo hayo yakiwakatisha tamaa vijana walioamini kuwa wanaweza kuchagua viongozi ambao wangekuwa wasemaji wao.

Alisema gharama za maisha zimepanda kutokana na kupaa bei za bidhaa huku kipato kikiwa hakijaongezeka, gharama za matibabu zikiwa juu kiasi cha wananchi wa kawaida wakishindwa kuzimudu wakati viongozi na matajiri wakienda nje ya nchi kupata matibabu ya uhakika.

Alisema hali ya ubora wa elimu kwa shule za serikali iko chini kiasi ambacho hakuna hata kiongozi wa serikali anayeweza kuwapeleka watoto au wajukuu zake kusoma katika shule hizo.

Alisema kutokana na hali hiyo, watu wengi wamejengewa matumaini hewa na wanasiasa na viongozi wa dini. Kutokana na shida zilizokithiri, waumini wengi wamekuwa mateka wa viongozi wa dini wenye tamaa ya kuvuna pesa kutoka kwao kwa njia ya njia za ulaghai huku watawala wakitoa ahadi nyingi hewa za kuboresha maisha huku hali ya maisha ikizidi kuzorota.

"Unafiki utajengeka katika nyumba zetu za ibada, vyama vya siasa, katika serikali na jamii yote kwa ujumla. Hivyo, ni wajibu wetu sote kuanza kujihoji na kutafuta majawabu ya maswali yanayoikabili jamii yetu," alisema.

Alisema katika mazingira hayo, umma wa Watanzania unaingia kusherekea Krismasi ya mwaka 2024 ukiimba ujumbe wa wimbo wa gloria bila kufahamu ni kwa namna gani Yesu anaweza kuwatoa katika changamoto za kimaisha wanazopitia sasa.

"Inawezekana uchechemuzi ambao Yesu aliufanya wakati wa huduma yake ilikuwa ni sehemu ya ukombozi. Yeye alikemea sheria na mifumo kandamizi sambamba na tamaduni zilizokuwa zinawatia watu umaskini ikiwemo ya kutokutenda mambo mema siku ya Sabato," alisema

## Samia awachangia mil. 10/- bodaboda

**Na Allan Isack,** ARUSHA

RAIS Dk.Samia Suluhu Hassan ametoa Sh. milioni 10 kwa uongozi wa Chama cha Waendesha Bodaboda Wilaya ya Arusha, kwa ajili ya kuwawezesha kukamilisha utaratibu wa kuanzisha chama cha ushirika.

Licha ya Rais kutoa fedha hizo, pia ametoa pikipiki mbili kwa chama hicho zitakazotumiwa na viongozi ngazi ya wilaya na mkoa kwa shughuli ya kuwatembelea wanachama na kusikiliza kero zinazowakabili na kuzitatua.

Fedha hizo zilikabidhiwa jana jijini hapa na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Mohamed Kawaida, wakati wa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Waendesha Bodaboda Wilaya ya Arusha, ulioambatana na uzinduzi wa mfumo wa kidijitali wa utambuzi wa wanachama.

Alisema Rais amefikia uamuzi wa kutoa fedha hizo kwa kuwa awali waendesha bodaboda hao walikosa fedha za kukamilisha utaratibu wa kuanzisha ushirika huo.

Pia kiongozi huyo aliliagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kufanya uchunguzi wa kupotea kwa zaidi ya Sh. milioni 200 zinazodaiwa kuchukuliwa na baadhi ya viongozi wa bodaboda awamu iliyopita.

Vilevile, aliwataka waendesha bodaboda kujisimamia na kuacha kufanya matukio yasiyofaa yakiwamo kutumia dawa za kulevya na kunywa pombe kupita kiasi wakati wakitekeleza majukumu yao.

Aidha, Kawaida alilitaka kundi hilo la usafirishaji kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi kwa watu wanaotumia mwavuli wa bodaboda na kuvunja sheria. Katika hatua nyingine, waendesha bodaboda hao, waliiomba serikali kupunguza gharama za ukataji wa leseni ya udereva kufikia Sh.30,000 kwa kuwa hadi mchakato kukamilika unawagharimu Sh.99000 ili kila mmoja aweze kumiliki leseni.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, alitoa Sh. milioni 10 kuchangia mfuko wa chama cha bodaboda wilaya ya Arusha.

Akiwasilisha malalamiko yake mbele ya Kawaida, Mbunge huyo alionesha kusikitika kwa wahusika wanaodaiwa kuchukua na kutafuna Sh. milioni 200 za umoja huo kutokukamatwa hadi sasa na imeshapita miaka minne. Mwenyekiti wa Waendesha Bodaboda Wilaya ya Arusha, Shwaibu Hamisi, alisema wilayani humo wana bodaboda 12,500 huku Mkoa huo, ukiwa na bodaboda 26,000.

Mwenyekiti wa Bodaboda na Bajaji Taifa, Said Chenja, alisema kazi ya bodaboda si ya laana na wanamshukuru Rais kwa kuwapunguzia faini kutoka Sh.30,000 hadi Sh. 10,000 na pia pikipiki za magurudumu matatu faini zake zimepunguzwa.

# Mwinyi awahimiza viongozi kauli maridhawa kuepusha mifarakano

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema viongozi wana wajibu wa kuhubiri amani na umoja kwa kutamka mambo mema ili kuepuka mifarakano katika jamii.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana wakati akitoa salamu kwa waumini wa dini ya Kiislam kwenye ibada ya sala ya Ijumaa, Masjid Baaruut, Mwembe Mchomeke, Wilaya ya Magharibi B, mkoa wa Mjini Magharibi.

Kwa mujibu wq taarifa iliyotolewa na Idara ya mawasiliano, Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema viongozi wa dini na wanasiasa wana kila sababu ya kutokuwa sehemu ya kuvuruga amani kwa kuwa kauli zao zinasikika na wengi kuwa na nguvu, hivyo ni vyema wakawa mstari wa mbele kuhubiri amani, umoja na mshikamano kwenye jamii.

Alhaji Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa ili nchi iwe na mazingira mazuri ya kuleta maendeleo, kila mmoja kwa nafasi yake, hususani viongozi, wanalazimika kutamka kauli zenye kujenga, kuleta umoja na mshikamano.

Alisema bila mambo hayo, nchi haiwezi kupiga hatua kimaendeleo.

Kuhusu malezi na maadili, Dk. Mwinyi aliwasisitiza wazazi na walezi kuwaonya na kuwakemea watoto na vijana pale wanapofanya mambo kinyume cha maadili, silka au utamaduni.

Alisema dunia ina mabadiliko mengi yanayowaharibu watoto, yakiwamo utandawazi, matumizi ya dawa za kulevya, wizi na ubadhirifu wa mali za umma, hali inayotaka mkazo maalum kwa kuhimiza maadili mema na kuwakataza watoto ili kurudi katika maadili mema na misingi ya uislam.

Akihutubia ibada ya sala hiyo, Khatib Sheikh Ahmeid Khamis alisema wazazi na walezi wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwamiliki watoto katika njia nzuri za malezi yanayozingatia maadili ya dini ili kuirejeshea Zanzibar sifa na hadhi yake ya kuwa nchi yenye maadili mema.

Katibu Mtendaji Ofisi ya Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Mfaume, alisema wazazi na walezi wana wajibu wa kuweka utaratibu maalumu wa kuwahoji watoto ili kujua mambo wanayokabiliana nayo kwa dhamira ya kuwajenga mapema kwa imani na maadili.

Pia aliihimiza jamii kuunganisha nguvu ya pamoja kwa kuwa suala la malezi si la mtu au taasisi moja, hivyo lazima watoto wafundishwe tawhid kwa dhamira ya kumjua mola wao.

Alisisitiza kuwa zawadi nzuri zaidi anayopaswa mzazi kumpa mtoto wake ni malezi bora, elimu na adabu ili nchi iwe na watu wenye nidhamu na hatimaye kuwa na taifa bora.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mwendesha pikipiki akiwa amepakia kuku kwenye tenga na mteja wake eneo la Lugoba wakielekea Chalinze mkoani Pwani kwa ajili ya kuuza hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# DC awapa mbinu wananchi za kukacha mikopo 'kausha damu'

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Tarime, Edward Gowele, amewataka wananchi wilayani hapa kujiweka kando na mikopo umiza maarufu kama 'kausha damu' kwa kutumia taasisi za fedha zinazotambuliwa zikiwamo benki kupata mikopo iliyodhibitiwa viwango vya riba na masharti.

Amesema benki zote na taasisi za fedha halali zinazotoa huduma katika wilaya hiyo zimeweka masharti nafuu ikiwamo kutoa riba nafuu kuruhusu wananchi wengi kuachana na mikopo umiza inayodidimiza uchumi wao.

Gowele alitoa wito huo wakati akifungua tawi jipya la benki ya CRDB katika mji wa mpakani, Sirari, na kukemea tabia ya baadhi ya taasisi kutoa na kuweka fedha kutoza wananchi riba zaidi ya asilimia 50.

Alisema serikali inashirikiana na taasisi za kifedha zikiwamo benki zote ili wajasiriamali wadogo ambao hawajafikia vigezo vya kukopa fedha nyingi kupata uwezeshaji kupitia mikopo ya kawaida ili kuwanusuru na mikopo yenye masharti magumu inayowarudisha nyuma kimaendeleo na kimaisha.

"Ni rai yangu kwamba wananchi kutoka makundi yanayopendelewa ya wanawake, vijana na walemavu watarejesha fedha wanazokopa kwa wakati ili zirejee katika mzunguko na kuwezesha wengine kukopa kwa urahisi, "alisema.

Uwapo wa taasisi hizo karibu na wananchi, alisema zimewezesha kufanyika malipo kwa njia za kidijitali na ulipaji kodi na tozo za serikali kwa ajili ya huduma mbalimbali ikiwemo umeme na maji na serikali kukusanya mapato.

Meja Gowele alizitaka benki wilayani Tarime kubuni mipango ya kutoa elimu kwa umma kuhusu utunzaji akiba na ujasiriamali kuhakikisha fedha zao zinakuwa salama na kuongeza nidhamu katika matumizi

Ofisa Mkuu Usimamizi Biashara wa CRDB, Boma Raballa, alisema hivi sasa benki hiyo inaendesha mpango wa kuuza hati fungani za miundombinu ya Samia ili kuwezesha kujenga miundombinu ya barabara.

Alisema kiasi cha uwekezaji kinaanzia Sh.500,000 na hakina kikomo cha juu cha uwekezaji na mwekezaji atapewa faida ya asilimia 12 kila robo ya mwaka na haitakuwa na kodi ya zuio.

"Tunawashauri wananchi wote waliowekeza katika hati fungani hiyo watumie fursa hiyo kama dhamana ya kupata mkopo katika benki au taasisi yoyote inayotambulika hapa nchni kwa kuwa inawezekana," alisema.

**-Imeandaliwa na Ambrose Waitangwa, Samson Chacha (TARIME)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi fainali AFCON 2025 yasiwe ya zimamoto

**ASANTE** Mungu, ndio neno tunalostahili kusema Watanzania na hasa mashabiki na wadau wa mpira wa miguu hapa nchini kutokana na mafanikio ambayo timu zetu zimepata.

Baada ya kumshukuru Mungu, ni wakati mwingine wa kuwapongeza viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), walioko chini ya Rais, Wallace Karia kwa kuongoza timu zake kufanya vyema katika mechi za kusaka tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya CAF.

Inajulikana wazi, jitihada hizi hazikuwa za TFF peke yake, Serikali ya Dk. Samia Suluhu Hassan, ilikuwa karibu katika kuhakikisha mafanikio hayo yanapatikana na Watanzania wanapita kifua mbele dhidi ya wapinzani wao.

Kwa mara ya kwanza, Tanzania imekata tiketi ya kushiriki katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa timu zake saba, na zimefanya hivyo katika kipindi cha mwaka 2024, ambao umebakiza siku chache ili kumalizika.

Timu saba za Tanzania zitapeperusha bendera ya nchi katika fainali tofauti, na fainali hizo zote zikitarajiwa kuchezwa mwakani.

Timu ya kwanza ni ile ya soka (Taifa Stars), ambayo itashiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), huko nchini Morocco, timu hii ilifuzu kibabe baada ya kuchukua pointi tatu za ugenini dhidi ya Guinea, na ikazibeba za nyumbani katika mchezo wake wa mwisho.

Wawakilishi wengine wa Tanzania watakaoshiriki mashindano ya Afrika ni kikosi chenye wachezaji wanaocheza ligi za ndani na fainali zao maarufu hujulikana kwa jina la CHAN, fainali hizi zitafanyika hapa nyumbani na hii ni sehemu ya maandalizi ya kuwa wenyeji wa fainali za mwaka 2027.

Twiga Stars, Timu ya Taifa ya Wanawake, pia imefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika, awali fainali hizi zilitarajiwa kuchezwa mwaka huu huko Morocco, lakini kwa sababu ambazo ziko nje ya CAF, zilisogezwa mbele na sasa zitafanyika kuanzia Julai 6 hadi 26, mwakani.

Vijana wenye umri chini ya miaka 20 maarufu Ngorongoro Heroes pia wamefuzu kushiriki fainali za AFCON U-20, Serengeti Boys wamekata tiketi ya kwenda kuwania taji la Afrika la AFCON U-17 pamoja na wadogo zao U-15 ambao watakwenda kupambana kwenye michuano ya Shule ya Afrika.

Kufuzu ni jambo moja, lakini kufanya vizuri katika mashindano hayo ni jambo lingine. Ili timu zetu ziende katika fainali hizo bila wasiwasi, zikijiamini na zikiwa na morali, ni lazima zipate maandalizi mazuri na maandalizi hayo yafanyike mapema.

Huu ni wakati wa Serikali na viongozi wa TFF kuanza mapema maandalizi kwa sababu ile ahadi ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' ya kutaka kuweka rekodi ya kuchukua ubingwa wa CHAN na kuvuka hatua ya makundi kwenye fainali za AFCON 2025 inatimia, basi ni kuanza kuziandaa timu hizi mapema.


Maandalizi ya zimamoto kamwe hayatatusaidia Watanzania, bado tusiamini wachezaji wetu wanaweza kuwa tayari kwa mashindano kwa kuwaweka pamoja siku chache kama wanavyofanya wenzetu ambao vikosi vyao vinaundwa na asilimia kubwa ya nyota wanaosakata kandanda la kulipwa Ulaya.

Hata ikiwezekana ligi kusimama, huu ndio wakati ambao hatutakiwi kukosea, tunatakiwa tuwe na mikakati ya kubeba ubingwa na kumrejeshea furaha Rais Samia ambaye amekuwa shabiki na mdau namba moja wa michezo hapa nchini.

Wakati Serikali ya Tanzania ikijipanga kuziandaa vyema timu, wachezaji watakaopata nafasi ya kuitwa katika timu hizo wanatakiwa kufahamu hiyo ni fursa yao kubwa ya kujiweka sokoni kwa kupandisha thamani zao.

Mashindano ya AFCON yamekuwa ni daraja kwa wachezaji wa Afrika kuonekana na makocha wa Ulaya, hivyo nyota wetu wajiandae kucheza kwa juhudi ili kuipa nchi matokeo chanya na vile vile kujitafutia soko katika timu za nje.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera TFF kuipeperusha Tanzania kibabe CAF 2024

**ZIMESALIA** siku tatu tu kumaliza mwaka 2024 na haitarejea tena kwenye dunia hii, ila utabaki kwenye kumbukumbu.

Katika rekodi ambazo zitawekwa ni umekuwa mwaka wa mafanikio makubwa katika medani za michezo hasa kwenye soka.

Kwanza kabisa, tunaanza kwa klabu mbili za Tanzania, Simba na Yanga kutinga hatua za makundi ya michuano ya kimataifa inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Yanga imetinga hatua ya makundi kwenye Ligi Mabingwa Afrika, huku Simba ikiwa ndani iachuana katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa miaka ya hivi karibuni imeonekana ni kawaida kwa timu za Tanzania, hasa Simba ambayo imeingia mara nyingi zaidi na sasa Yanga imeanza taratibu kuzoea kuingia hatua hiyo.

Ukiacha hilo, mwaka 2024 umeonekana kutia fora kwenye timu za taifa za soka, timu saba zimefanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali za mataifa ya Afrika.

Timu ya Taifa ya vijana chini ya miaka 17, Serengeti Boys, ndio ilikamilisha idadi ya timu za Tanzania zitakazokwenda kucheza fainali za AFCON U-17, zitakazofanyika nchini Morocco mwakani.

Hii ni baada ya kuichapa, Sudan Kusini mabao 4-0, katika mchezo wa nusu fainali katika michuano ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Tanzania pia mwaka huu ilifuzu fainali za mataifa ya Afrika kwa walemavu (BAFCON), yaliyofanyika mwaka huu nchini Misri.

Kikosi cha timu ya taifa chini ya miaka 15 nacho lilifanikiwa kufuzu fainali za mashule barani Afrika, huku Tanzania ikiwa mwenyeji.

Timu ya taifa chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes)nayo haikuwa nyuma, kwani ilifuzu fainali za AFCON, ambazo zinatarajiwa kufanyika Ivory Coast. Kikosi cha timu ya taifa ya wanawake, Twiga Stars nacho waka huu kilifanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali za mataifa ya Afrika (WAFCON), zinazotarajiwa kuchezwa Morocco. Kama vile haitoshi Tanzania imepeleka fainali timu mbili za soka wanaume, moja ya wachezaji wa ndani ya nchi na nyingine ni ya jumla.

CHAN, michuano ya wachezaji wa ndani, Stars ilifuzu fainali hizo zinazotarajiwa kupigwa mwakani katika nchi tatu za Tanzania, Kenya na Uganda.

Taifa Stars, timu kubwa ya soka Tanzania yenye wachezaji wote wa ndani na nje, imefanikiwa kufuzu (AFCON), zinazotarajiwa kuchezwa Morocco pia.

Kwa hili hatuwezi kupita bila kulipongeza Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), chini ya uongozi wa, Rais Wallace Karia.

Uongozi wa Karia umeonekana kujipambanua si tu kuibua vipaji vya soka la vijana wanaume na wanawake, lakini pia kutengeneza vikosi imara vya kila timu ya taifa na umri wake, zinazokwenda kuleta ushindani kubwa barani Afrika. Nadhani umekuwa na mpango mkakati sahihi na wakati sahihi, pamoja na kuchukua vijana wenye umri sahihi na vipaji sahihi pia.

Ni uongozi ambao umekuwa ukiamini mchezaji mwenyewe kupambana kwa uwezo wake na si kuwekeana kanuni za wazawa kupata upendeleo wa kucheza na kuzuia wageni.

Hii imefanya pia wachezaji wa Kitanzania kuanza kupambana bila kutegemea mbeleko ya uzawa.

Hivi karibuni nilimsikia akikataa ushauri wa baadhi ya wacheambuzi kuwepo kwa kanuni ya makipa watupu wa kizawa, akiwaambia hata wao wazawa wanahitaji makipa wageni ili na wao wajiboreshe na kwa maana hiyo Tanzania itapata makipa wazuri.

Akasema hawezi kuipangia timu kumweka kipa mzawa, badala yake makipa wote wanatakiwa kuonyesha ushindani na makocha wapange bila kujali ni Mtanzania au mgeni, badala yake kiwango ndicho kitaamua.

Na hii ni baada ya pia mwanzoni mwa msimu baadhi ya wadau kutaka kupunguzwa kwa wachezaji 12 wa kigeni wanaohitajika kikanuni, lakini kiongozi huyo na baadhi ya wadai walipinga kwa madai watapunguza msisimko wa ligi, kwani moja ya vitu vinavyoifanya Ligi Kuu Tanzania kuvutia ni kuwepo kwa wachezaji mbalimbali kutoka bara la Afrika, na hata mabara mengine duniani.

Karia na TFF yake inastahili pongezi kwa kuongoza kwa kutofuata mihemko ya mashabiki na wachambuzi, matokeo yake Tanzania imekuwa ikipiga hatua.

Hongera TFF, ni nyinyi mlioipa sifa Tanzania kumaliza mwaka 2024 kwa kishindo, timu zake saba kufuzu michuano ya CAF ambayo miaka ya nyuma wadau na mashabiki wa soka walikuwa watazamaji tu.

# Wizara Afya yasubiri mapendekezo ubora chanjo kudhibiti malaria

**Na Grace Mwakalinga**

WIZARA ya Afya inasubiri mapendekezo kutoka Kamati ya Kitaifa ya Masuala ya Chanjo (NITAG), ambayo itapitia na kutoa maoni kuhusu gharama, ubora na upatikanaji wa chanjo za kudhibiti malaria nchini.

Meneja wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kutoka Wizara ya Afya, Dk. Samwel Lazaro, alisema kuwa chanjo mbili za malaria - RTS, S na R21 - zinaoendelea kupitia mchakato wa mapitio, zinasubiri kupitishwa na Timu ya Wataalam ili kuanza kutumika rasmi nchini.

Dk. Lazaro alifafanua kuwa Wizara ya Afya inategemea maoni ya kitaalam kutoka Kamati ya Kitaifa ya Masuala ya chanjo ili kufanikisha utoaji wa chanjo hizo, hasa kwa watoto chini ya miaka mitano, ambao ni waathirika wa ugonjwa wa malaria.

Alisema chanjo ya RTS, S, inayotengenezwa na kampuni ya GSK kutoka Ubelgiji, bado haijakidhi vigezo vya usajili vinavyotakiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), na kwamba serikali inasubiri mtengenezaji kumaliza mchakato wa usajili.

Chanjo ya R21, ambayo ilipata usajili rasmi Julai 2024, pia inahitaji kupitia mchakato wa tathmini ya kitaalam kutoka kwa Kamati ya Kitaifa ya Masuala ya Chanjo kabla ya kuanza kutumika.

"Tunazingatia miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu utolewaji wa chanjo na tunasubiri ripoti ya Kamati ya Masuala ya Chanjo ili kupata ushauri wa kitaalam kuhusu ubora, gharama, upatikanaji na usalama wa chanjo hizi," alisema Dk. Lazaro.

Akizungumzia jitihada za kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa malaria, alisema takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2022, zinaonesha kuwa kati ya watu 100, ni wanane pekee waliobainika kuwa na vimelea vya malaria.

Alisema hiyo ni hatua kubwa ikilinganishwa na miaka ya 1990, kati ya watu 100, watu 50 hadi 60 walikuwa na maambukizi ya ugonjwa huo. Dk. Lazaro alisema kuwa hatua hizo za kupunguza maambukizi ni matokeo ya juhudi za pamoja za serikali, pamoja na mikakati ya kinga na matibabu, alisema bado kuna umuhimu wa kuendelea na juhudi za kudhibiti ugonjwa huo, hasa kupitia utoaji wa chanjo.

Alisema Serikali pia inaendelea kuimarisha juhudi za kinga na matibabu ya malaria, katika mwaka wa fedha 2024/2025, kiasi cha Sh. bilioni 10 kimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa za viuadudu katika kiwanda cha kuzalisha viuadudu vya kuua viluilui vya mbu wanaoeneza malaria kilichopo Kibaha, mkoani Pwani. Aidha, Shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa pampu za kunyunyizia viuadudu vya kibaiolojia.

Alisema kuwa kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), ugonjwa wa malaria husababisha vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa asilimia 75 hadi 80.

Kutokana na hali hiyo, serikali inaendelea kutoa vyandarua vya mbu kwa watoto na wajawazito, kuhamasisha usafi wa mazingira, kufukia madimbwi yenye maji yaliyotuama na kutumia viuadudu vya kibaiolojia kudhibiti viluilui vya mbu.

"Serikali pia inaendelea kutoa matibabu bure kwa wagonjwa wa malaria na inahimiza wananchi kupima afya zao kabla ya kutumia dawa. Si kila homa ni malaria, hivyo tunawasihi wananchi kupima na kuhakikisha wanakamilisha dozi zao ili kuepusha usugu wa dawa," alisisitiza Dk. Lazaro.



Mbunge wa Iramba Mashariki, Francis Mtinga, akipanda mti jana katika maeneo ya Shule ya Sekondari Mwenge iliyopo Manispaa ya Singida. Mbunge huyo ambaye ni miongoni mwa wanafunzi waliosoma katika shule hiyo 1991-1994 aliungana na wenzake kwa ajili ya kupanda miti 1000 katika shule hiyo ili kutunza mazingira. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wadau mazingira washauri serikali mikakati kukabiliana athari za ukame

**Na Jenifer Gilla**

WATAALAM na wadau wa mazingira nchini wameishauri wizara kuja na mikakati ya pamoja ya kukabiliana na athari za ukame ikiwamo teknolojia za kisasa za kuvuna na kuhifadhi maji, chakula na kuhamasisha uhifadhi wa uoto wa asili.

Hayo yamesemwa ikiwa ni wiki mbili tangu ripoti iliyotolea na Mpango wa Kudhibiti Kuenea kwa Jangwa na Ukame duniani (UNCCD), iliyoitwa Tishio la Kimataifa la Kukauka kwa ardhi; Mwelekeo wa Ukame wa Kikanda na Ulimwenguni na Makadirio ya Baadaye, kuzitaja nchi za Tanzania na Sudan Kusini, kuwa zinaelekea kwenye ukame kwa kasi kubwa ikilinganishwa na nchi nyingine ulimwenguni.

Ripoti hiyo iliyozinduliwa Desemba 9, mwaka huu katika mkutano wa 16 nchi wanachama wa UNDCC (COP 16) uliofanyika Riyadh, Saud Arabia, Novemba 30 hadi De semba 14, mwaka huu, (COP16) ilionyesha wasiwasi kuhusu ongezeko la ukame ulimwenguni. Kwa mujibu wa ripoti hiyo kama hali ya ukame ikiendelea kuongezeka itasababisha madhara makuwa ikiwamo uharibifu wa mifumo ya ikolojia ikiwamo ardhi kukosa rutuba na kusababisha kudorora kwa kilimo.

Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, alisema ni vigumu kuzuia ukame usitokee nchini kwa sababu unachochewa na athari za mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaikabili dunia kwa sasa.

Alisema ili kupunguza makali ya athari za ukame na jangwa kama nchi, wizara zinapaswa zijipange na kufanya kazi kwa kushirikiana na kuja na mikakati ya kuleta uhimilivu.

Alitaja baadhi ya mikakati hiyo kuwa ni kuhakikisha kuwa kipindi ambacho mvua zipo za kutosha uzalishaji wa chakula uwe wa juu ili kihifadhiwe cha kutosha kitumike kipindi ambacho uzalishaji ni mdogo kutokana na mvua kuwa chache.

> **Pia, inapaswa kujiandaa na kuja na mbinu bora za kutatua migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na ukame ikiwamo ya wafugaji na wakulima akisisitiza njia hizo zinapaswa kuwa za kuyanufaisha...**

Alisema pia serikali na wadau wahamasishe teknolojia ya kisasa ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kulisha mifugo ili kuepuka migogoro inayoweza kutokea kutokana na ukame kama migogoro kati ya wakulima.

Pia, inapaswa kujiandaa na kuja na mbinu bora za kutatua migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na ukame ikiwamo ya wafugaji na wakulima akisisitiza njia hizo zinapaswa kuwa za kuyanufaisha makundi yote kwa usawa.

Aliishauri pia serikali ijipange kudhibiti vijana kukimbilia mijini na kusasababisha msongamano mkubwa wa watu na kuongeza athari za ukame kama vile maji kuadimika.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mikakati ya Maendeleo Endelevu (TSDI), Fredy Kwezi, alisema licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa mazingira kupanda miti ili kudhibiti athari za mabadiliko ta tabianchi yanayochochea ukame, matokeo bado hayaridhishi.

Alitaja sababu za kutoridhishwa kwa matokeo hayo kuwa wadau hao wamejikita zaidi kwenye kupanda miti, lakini hawarudi kuangalia kama miti hiyo imestawi au la na namna ya kuitunza.

Fredy aliyehudhuria COP16 akiiwakilisha nchi, alisema hali hiyo inasababisha miradi mingi ya upandaji miti kufeli kwa sababu wadau wa shughuli hiyo wakishapanda mti wanapiga picha na kurusha mitandaoni na kuishia hapo.

Alisema njia sahihi ya kupanda miti ikastawi na kuleta matokeo chanja ni kushirikisha wataalam ili kufahamu ni aina gani ya miti ipandwe katika eneo fulani. "Kwa sababu miti inayostawi vizuri Njombe huwezi kuipanda Dar es Salaam, na inayostawi vizuri Pwani huwezi kwenda kuipanda Mbeya," alisema.

Alitaja pia njia ya mpango wa matumizi bora ya ardhi kama suluhisho la kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa ikitumika vizuri inasaidia kuzuia vivutio vya ukame kama vile mmomonyoko wa udongo.

Mtaalam wa mabadiliko ya tabianchi Nyendo Kinyonga, alisema kuna haja ya kutoa elimu kuanzia ngazi ya familia hadi kitaifa kuhusu ukame na visababishi vyake na namna ya kukabiliana nao, ili jamii ichukue nafasi yake kujikinga badala ya kutegegemea mamlaka.

Alisema suala hili liachiwa mamlaka za kiserikali pekee kama vile Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na Wakala wa Misitu matokeo hayatakuwa tarajiwa na ukame utazidi kuongezeka na kwamba kila mmoja anapaswa awajibike kwa nafasi yake.

"Kwa mfano kwa sasa hivi kuna changamoto ya wakulima kusafisha mashamba kwa kuyachoma moto, hii izalisha sana hewa ya kaboni inayochochea athari za mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo joto kali na kusababisha ukame," alifafanua.

Alishauri pia wakulima wajikite kwenye kilimo cha zamani ambacho kilikuwa hakitumii mbolea kutokana na matumizi ya viuatilifu kuharibu udongo, na kuchochea ukame.

Mkugenzi wa Taasisi ya Human Dignity and Environmental Care Foundation (HUDEFO), Sarah Pima, alisema jitihada za pamoja zinahitajika katika nchi za Jangwa la Sahara ili kukabiliana na ukame.

Alisema kwa upande wa Tanzania kunahitajika sera madhubuti za kukabiliana na jangwa ikiwamo kuongeza kiwango cha kuhifadhi uoto wa asili na misitu iliyopo badala ya kuegemea kwenye kupanda miti pekee.

Aliwasihi wananchi kulichukuliwa suala la jangwa na ukame kwa uzito kwa sababu athari zinazidi kuongezeka, mikakati ya kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi itekelezwa sasa badala ya kusubiri hali ikiwa mbaya.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, ukame ni chanzo kikuu cha uharibifu wa ardhi, ukiharibu takriban asilimia 40 ya ardhi yenye rutuba duniani, hivyo kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa kilimo na uhaba wa chakula.

Ilieleza pia barani Afrika, kuongezeka kwa ukame kumehusishwa na kupungua pato la taifa kwa asilimia 12 kati ya mwaka 1990 na 2015, jambo linaloonyesha changamoto za kiuchumi zinazosababishwa na uharibifu wa ardhi.

Kupitia michango iliyoamuliwa Kitaifa (Nationally Determined Contribution - NDC), Tanzania imeahidi kupunguza uzalishaji wa gesi chafuzi kwa kiwango cha asilimia 30 hadi 35 katika sekta zote za uchumi, ikilinganishwa na hali ya Kawaida ifikapo mwaka 2030.

Hali hiyo inatarajiwa kupunguza takriban tani milioni 138-153 za kaboni dayoksaidi (MtCO2e) kwa jumla, kutegemeana na maboresho ya ufanisi wa msingi, sambamba na ajenda yake ya maendeleo endelevu.

# Bil. 3.1/- kutumika kwa mpango lishe

**Na Steven William,** MUHEZA

DIVISHENI ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, kwa mwaka 2025/26 inatarajia kukusanya na kutumia Sh. bilioni 3.168 ili kugharamia utekelezaji wa mpango na bajeti.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Fani Mussa, alisema hayo mapema wiki hii katika kikao cha maandalizi ya mpango kabambe wa afya kwa mwaka 2025/26 kilichofanyika katika ukumbi wa Hospitali ya Wilaya ya Samia.

Alisema mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa Sh. 876,627,203 ikijumuisha mapato ya vituo vya huduma za afya yanayokadiriwa kufikia Sh. 462,700,000.

Dk. Mussa alisema katika mwaka 2023/24, Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe ilikadiria kupata mapato nakutumia Sh. bilioni 3.598. Katika kipindi hicho, divisheni ilipokea Sh. bilioni 3.728 sawa na asilimia 103.6 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Alisema kiasi hicho kinajumuisha Sh. 389,749,812.78 mapato ya ndani sawa na asilimia 223.63 ya lengo la mwaka la Sh. 174,280,000.

Dk. Mussa alisema katika kipindi hicho, divisheni imetumia Sh. bilioni 3.426 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi ya divisheni na Sh. milioni 4.59 zilivuka mwaka.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, alisema divisheni imepokea Sh. 767,441,921.08 na kati ya kiasi hicho, Sh. 192,528,604 ni mapato ya makusanyo ya vituo vya huduma za afya ndani, sawa na asilimia 52.6 ya lengo.

Alisema mwaka 2025/26, divisheni itaendelea kutekeleza vipaumbele 13 vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Mpango Kabambe wa Afya kwenye (CCHP Toleo la 5 la mwaka 2020.) na maelekezo mahususi ya Mwongozo wa Mipango na Bajeti wa Serikali wa mwaka 2025/26.

Mgeni rasmi katika mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Issa Msumari, alisema kumekuwa na tabia ya watumishi wa idara ya afya wakati serikali inapeleka fedha katika sekta ya afya, zinapelekwa katika vituo lakini hazitumiki mpaka mwaka unapita halafu zinarejeshwa tena serikali kuu, hivyo mtindo huo hataki kuusikia tena.

Alisema lazima watumishi wa Afya wajenge umoja wa kujaliana na kuthaminiana katika kazi na kwamba mtumishi anapotakiwa kupewa stahiki yake ya posho kutokana na mshahara wake apewe.

# Wasiopeleka watoto sekondari waonywa

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

SERIKALI wilayani Masasi mkoani Mtwara imeendelea kusisitiza wazazi na walezi ambao watoto wao wameteuliwa kujiunga na kidato cha kwanza, 2025 kuhakikisha wanawapeleka shuleni kuanza masomo kwa wakati.

Sambamba na msisitizo huo, imeonya kuwa mzazi na mlezi yeyote ambaye atabainika kushindwa kufanya hivyo, sheria itachukua mkondo wake.

Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Lauteri Kanoni, alitoa agizo na onyo hilo juzi alipokuwa akizungumza na waumini wa Kanisa Katoliki Jimbo la Tunduru wakati wa Misa ya Krismasi na kuelekea mwaka mpya 2025

Kanoni amesema mwezi ujao (Januari) shule zote zinafunguliwa, hivyo kila mzazi au mlezi ambaye mtoto wake amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza ahakikishe anaripoti shuleni na tena kwa wakati ili kuanza masomo.

"Baadhi ya wazazi na walezi wilayani Masasi wamekuwa wakijikita sana katika mambo ya starehe kama vile vigodoro na kutumia fedha nyingi sana lakini ikifika suala la kumsomesha mtoto, wanasema hawana fedha. Sasa hii mwisho tutachukua hatua kali," alisema Kanoni Mkuu huyo wa wilaya alisema wako baadhi ya wazazi na walezi wamekuwa kikwazo katika kuwapeleka watoto wao shuleni na badala yake kuamua kuwaoza, kuwapeleka kufanya kazi za ndani mikoani kwa kisingizio cha kukosa fedha za kuwasomesha.

> **"Baadhi ya wazazi na walezi wilayani Masasi wamekuwa wakijikita sana katika mambo ya starehe kama vile vigodoro na kutumia fedha nyingi sana lakini ikifika ....**

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali wilayani Masasi haitosita kuchukua hatua kali kwa wazazi na walezi ambao watashindwa kuwapeleka watoto wao kuripoti shuleni wakati.

Alisema kila mtoto ambaye ameteuliwa kujiunga na sekondari ni haki ya kwenda shuleni kupata elimu, hivyo wazazi lazima watambue umuhimu wa elimu.

Kanoni alisema serikali ya wilaya ya Masasi Septemba, mwaka huu, ilifunga mkataba wa kisheria na kila mzazi na mlezi kuhakikisha kila mtoto aliyefaulu kwenda sekondari anaripoti shuleni kuanza masomo.

Alisema sheria inambana mazazi iwapo atashindwa kumpeleka mtoto wake shuleni basi achukuliwe hatua kwa mujibu wa mkataba huo ambao kila mazazi ametia saini ili kutii makubaliano hayo.

Owen Salum, mmoja wa mzazi, alisema wanampongeza mkuu wa wilaya kwa maagizo kwamba kila mzazi au mlezi anapaswa kufahamu nini maana ya elimu.

Mzazi mwingine, Rajab Shabani, alisema bado katika mikoa ya kusini kuna mwamko mdogo wa wazazi kuthamini elimu, hivyo kupitia agizo hilo la mkuu wa wilaya, itasaidia kuamsha ari kupenda elimu kwa jamii.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis (watatu kushoto) akitoa zawadi za Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya kwa niaba ya Rais Samia Suluhu katika Makao ya Watoto na Makazi ya Wazee Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yafanya ukaguzi wa kushtukiza, mabasi yanaswa kwa madereva wawili

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limefanya ukaguzi wa kushtukiza wa mabasi yaendayo mikoani katika eneo la Usagara mkoani hapa na kubaini ukiukwaji wa sheria ikiwemo mabasi yaendayo umbali wa zaidi ya saa nane kuendeshwa na dereva mmoja kinyume cha sheria.

Akiendesha ukaguzi huo uliokwenda sambamba na elimu ya usalama barabarani kwa abiria, madereva na wasaidizi wao, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mwanza, Mrakibu (SP) Sunday Ibrahim, alisema wamebaini mabasi mawili yanayokiuka agizo hilo na kuyakamata.

SP Ibrahim alisema magari hayo yamekamatwa pamoja na wamiliki wake kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kushindwa kutimiza masharti na kanuni inayowataka kuajiri madereva wawili kwa mabasi yanayosafiri umbali mrefu wa zaidi ya saa nane.

Alisema lengo la ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara kwa mabasi ya abiria yaendayo mikoani ni kuzuia ajali zinazotokana na uzembe wa madereva ambazo zimekuwa zikitokea hasa nyakati hizi za sikukuu.

Kadhalika, aliwataka abiria kuchukua hatua za kisheria dhidi ya madereva wanaokiuka sheria za usalama barabarani kwa kuendesha kwa mwendo kasi pamoja na kukiuka kanuni za barabarani.

SP Ibrahim aliwakumbusha abiria haki zao za msingi na kuwataka kutofumbia macho vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya madereva kwa kutoa taarifa Polisi.

Mmoja wa abiria, Donald Chakachaka, aliliomba jeshi hilo kuendelea kufanya ukaguzi wa kushitukiza mara kwa mara kwa kuwa imebainika kuwa baadhi ya madereva wamekuwa wanafuata sheria za usalama barabarani pale wanapowaona askari kitendo ambacho kinahatarisha maisha ya abiria na watumiaji wengine wa barabara.

"Nimelipokea zoezi hili kwa mikono miwili kwa sababu linatusaidia sisi wasafiri kutuepusha na ajali. Kwa hiyo nawapongeza polisi wako sawa," alisema abiria Mwajuma Hamis

Dereva wa kampuni ya mabasi Nyehunge, Hassan Maneno, alisema kwa sasa madereva wamepunguza baadhi ya tabia za uvunjifu wa sheria za barabarani ikiwamo vurungu za kuyapita magari mengine bila kuchukua tahadhari kutokana na hatua ambazo wamekuwa wakichukuliwa.



## HABARI DODOMA

# Mradi wa usimamizi taka watekelezwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Jiji la Dodoma inatekeleza mradi wa majaribio wa usimamizi wa taka za plastiki.

Lengo la mradi huo ni kuhamasisha njia ya ubunifu katika usimamizi kupitia dhana ya uchumi rejeshi ili kupunguza taka za plastiki mtaani.

Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Ally Mfinanga, alisema hayo juzi baada ya kutembelea na kukagua mradi huo kwa ushirikiano na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira uliopo Kata ya Chamwino Jiji la Dodoma.

Mfinanga alisema mradi huo unatarajiwa utawanufaisha wananchi na kuwawezesha jamii na vikundi vya usafi kufanya shughuli zao za ukusanyaji na usafirishaji wa taka kwa nia ya kuongeza thamani kupitia dhana ya uchumi rejeshi ili kutunza mazingira.

Ofisa mazingira huyo alisema kupitia mradi huo pia jamii itawezesha kuongeza thamani ya taka hizo zinazotokana na plastiki ili kufanya dhana nzima ya uchumi kuwa rejeshi badala ya kuonekana kuwa hazifai kwa matumizi yoyote.

Alisema wanategemea kuwa na mashine ambayo itatumika kusaga chupa za plastiki ambazo zitakuwa zimetoka mtaani, kwenye makazi, masoko, maeneo ya biashara,taasisi na sehemu ambapo vikundi hivi vya Kata ya Chamwino vinafanya kazi. "Lengo letu ni kusaga chupa za plastiki na kuzisafirisha kwenda Dar-es-Salaam kwa ajili ya kutengeneza bidhaa nyingine za plastiki ikiwa ni pamoja na vyombo vya plastiki kama vifaa vya umeme, samani na kadhalika.

"Tunatarajia uchumi wa vikundi vinavyo fanya shughuli hii kupanda kidogo kwa sababu kwa sasa wanafanya kazi ya kukusanya na kusafirisha taka, lakini kupitia mradi huu wa majaribio wa usimamizi wa taka za plastiki wanaenda kujiongezea kipato zaidi" alisema.

# Kata 11 zanufaika mil. 70/- za jimbo

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

KATA 11 kati ya 18 zilizoko katika Manispaa ya Singida zimenufaika kwa kujenga miradi mbalimbali kutokana na Sh. milioni 69.883 za mfuko wa Jimbo zilizotolewa na serikali katika mwaka wa fedha wa 2023/24.

Hayo yalibainika jana baada ya Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilipofanya ziara kutembelea miradi iliyotekelezwa katika Manispaa ya Singida kwa fedha hizo.

Diwani wa Viti Maalum, Margareth Malecela, alisema fedha za Mfuko wa Jimbo ni za serikali, hivyo kata au taasisi zilizobahatika kupata fedha hizo zizingatie ubora ili kuwezesha miradi kudumu kwa muda mrefu.

Malecela ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo alisema pia wakati wa utekelezaji wa miradi taratibu zote za kisheria na kikanuni hasa za manunuzi wakati wa matumizi ya fedha hizo lazima zizingatiwe. "Fedha za mfuko wa jimbo zinasimamiwa na kamati na ni hela inayotolewa kwa utaratibu haitoki mfukoni mwa mtu... ni fedha ya kuchochea maendeleo ndani ya halmashauri," alisema.

> **"Fedha za mfuko wa jimbo zinasimamiwa na kamati na ni hela inayotolewa kwa utaratibu haitoki mfukoni mwa mtu... ni fedha ya kuchochea maendeleo ndani ya halmashauri,"**

Mtendaji wa kata ya Ipembe, Futari Shauri, ambaye ni mwakilishi wa watendaji wa kata, alionesha kufurahishwa na seti za viti na meza vilivyotengenezwa katika shule ya sekondari Mughanga ambayo ni miongoni mwa shule zilizonufaika na fedha za Mfuko wa Jimbo. Mjumbe mwingine, Emmanuel Weda, ambaye ni Mtendaji wa Kata ya Mwankoko, alisema wanufaika wa fedha hizo wahakikishe wanazingatia ubora kulingana na thamani ya fedha iliyowekezwa katika mradi ili mradi uweze kudumu muda mrefu.

Aidha, wajumbe wa kamati hiyo walipongeza miradi iliyotekelezwa kwa kiwango chenye ubora na kushauri maboresho katika baadhi ya miradi na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia ubora ili mradi uweze kudumu kwa muda mrefu.



Mbunge wa viti Maalum Mkoa wa Singida,Aysharose Mattembe (kulia aliyevaa kilemba cha njano) akikabidhi vifaa vya ujenzi kwa viongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mkalama mkoani Singida. Vitu hivyo alivikabidhi kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa nyumba ya Katibu wa UWT Wilaya ya Mkalama jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wanafunzi 35 wapunguziwa adha kutembea masafa kwenda shuleni

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAHANDISI wasio na mipaka kutoka Marekani, wamekabidhi msaada wa baiskeli kwa wanafunzi 35 wa Shule ya Sekondari Banyibanyi wilayani Kongwa, ili kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kwenda shuleni na kurudi.

Wanafunzi waliokabidhiwa baiskeli hizo wanatoka kijiji cha Mkutani kilichoko wilayani humo ambao walikuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilomita saba kufika shule ya Banyibanyi.

Akizungumza baada ya kukabidhi baiskeli hizo, Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Kongwa, Magreth Temu, aliwashukuru wahandisi hao huku akisema wamesaidia kupunguza tatizo la wanafunzi hao kutembea umbali mrefu pamoja na kukosa baadhi ya vipindi.

"Nawashukuru sana wahandisi hawa wa (USA ENGNEERS WITHOUT BORDERS) kwa msaada huu waliotoa, wameonesha ushirikiano mkubwa dhidi ya viongozi wilayani hapa kwenye maendeleo katika sekta ya elimu," alisema Temu.

Pia alisema mbali na kutoa baiskeli hizo, wamejenga nyumba ya mwalimu, matundu 12 ya vyoo, miundombinu ya kuvuna maji ya mvua na chumba cha kompyuta kwa ajili ya kusaidia wanafunzi kusoma masomo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) katika Shule ya Msingi Mkutani.

Temu alisema viongozi wa wilaya ya Kongwa wamekuwa mstari wa mbele katika suala la maendeleo hususani kwenye elimu kwa kutoa kipaumbele kwa wanafunzi wanaotoka kijiji cha mbali kupata baskeli hizo kwa ajili ya kuwasaidia usafiri.

Ofisa elimu huyo aliwataka wazazi kuhakikisha wanazitunza baiskeli hizo ili ziwe na faida iliyokusudiwa na wafadhili waliojitolea kutoa msaada huo.

Diwani wa Hogoro, Mtwanga Sadala, aliwataka wenyeviti wa vitongoji kushirikiana na wazazi kushughulikia utoro wa wanafunzi mashuleni na kuwasihi wanafunzi kuwa na nidhamu kwa walimu na jamii kwa ujumla.

Alisema nidhamu kwa wanafunzi inajenga msingi bora wa kusoma kwa bidii masomo wanayofundishwa na kupelekea kupata ufaulu mzuri katika mitihani yao ya taifa ambayo hufanyika kila mwaka.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi waliopokea baiskeli hizo, Claudia Njijila wa Shule ya Sekondari Banyibanyi, alisema awali walipata shida ya kutembea umbali mrefu walichoka ikiwemo kushindwa kusoma vizuri hivyo baiskeli hizo zitawasaidia kuwahi shule na kupata muda mzuri wa kujisomea.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mkutani, Samwel Chidabile, alisema anashukuru Wahandisi hao kwani wamekuwa ni marafiki bora tangu mwaka 2017 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hiyo.

Alisema hadi sasa tayari wamepokea baiskeli 121 ambazo zinasimamiwa na kamati ya shule kuhakikisha zinakuwa salama na kutumika kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Banyibanyi.





## Waziri ahimiza weledi katika utendaji kazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHW), kutekeleza majukumu yao kwa weledi ili kupata takwimu sahihi zitakazosaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo.

Mazrui aliyasema hayo jana wakati akizindua mfumo wa kuingiza taarifa za afya za familia zitakazotembelewa na wahudumu hao (ZANCHIS) na kuwatambulisha rasmi wahudumu waliohitimu mafunzo ya muda mfupi ya kutoa huduma za afya ndani ya jamii katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul-Wakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema kupatikana kwa takwimu sahihi na kwa wakati kutaisaidia Wizara ya Afya kupanga mikakati yake ya kuimarisha afya na kuchukua hatua kwa haraka katika dharura zinazotokezea.

Aidha, aliwataka wahudumu hao kujikita katika maeneo yanayoonekana kuwa na miundombinu kidogo ili kuibua changamoto za afya zilizoko katika maeneo hayo na kufanyiwa kazi.

Pia aliwataka kulinda na kuheshimu utamaduni, mila na silka za familia wanazozitembelea ili kupata ushirikiano wa kutosha hatua inayodhihirisha mafanikio ya safari ya kuelekea katika malengo ya kutoa huduma za afya bora kuanzia ngazi ya jamii. "Nawaomba mwende kuyatumia mafunzo hayo na vifaa mlivyopatiwa ili kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za awali katika ngazi ya jamii kabla ya kufika kituo cha afya", alisema.

Waziri Mazrui pia alitumia fursa hiyo kuwataka masheha na maofisa afya wa shehia kuwapa ushirikiano mawakala hao wanapofika kutaka kutekeleza majukumu yao ndani ya shehia husika.

Mkurugenzi Idara ya Kinga na Elimu ya Afya, Dk. Salim Slim, alisema lengo la CHW ni kuwasaidia wananchi kupata huduma ya mwanzo wakiwa majumbani kwao na kuwasaidia kufika vituoni pale hali inapobidi.

Dk. Slim aliwataka wahudumu hao kutekeleza vyema majukumu yao ili kuleta mabadiliko chanya kwa sekta ya afya na jamii kwa ujumla.

Alisema wahudumu hao wanajukumu la kupita nyumba hadi nyumba kupata taarifa za afya za wakaazi wa kaya hiyo ili kubaini maradhi ya mripuko na kudhibiti kuenea kwa maradhi ndani ya jamii huku akiwasisitiza kuzituma taarifa hizo sehemu husika kwa wakati ili zifanyiwe kazi.

# ZRA yawatua wananchi ndoo kichwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Zanzibar (ZRA) imewatua ndoo kichwani wananchi wa kijiji cha Donde Kiungani kwa kuwachimbia kisima kwa ajili ya kupata huduma ya maji safi na salama, ikiwa ni sehemu ya mwezi wa shukrani kwa walipakodi.

Wakizungumza katika hafla ya ufunguzi wa kisima hicho iliyofanyika kijijini hapo, wananchi wa kijiji hicho walisema uwapo wa kisima hicho ni faraja kwao kwa sababu wameondokana na changamoto ya kutafuta maji kwa umbali mrefu huku kinamama wakiwa waathirika wakubwa.

Fatma Khamis, mmoja wa wananchi hao, alisema kabla ya uwapo wa kisima hicho walikabiliwa na changamoto ya huduma ya maji jambo ambalo liliwarudisha nyuma katika kushiriki harakati mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

"Maji ndiyo kila kitu katika maisha ya binadamu. Nilikuwa nikiamka asubuhi tu nawaza kwenda kutafuta maji hali ambayo ilinigharimu sana kwa sababu muda mwingi naupoteza huko bila ya kushiki kikamilifu katika shughuli zangu za kiuchumi," aisema Fatma.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, itahakikisha inaendelea kufikisha maendeleo katika maeneo yote ya Unguja na Pemba hususan huduma za maji, umeme, afya na elimu ili kuwawezesha wananchi kunufaika na maendeleo hayo.

Alisema maendeleo yote ambayo yanafanyika hivi sasa yanatokana na kodi zinatokana na wananchi wenyewe, hivyo aliwataka kushirikiana na serikali kudai risiti za kielektroniki na kuiwezesha serikali kufanya mambo makubwa zaidi. Pia alisema zinasaidia kuleta maendeleo kwa nchi na wakiona barabara, maji, umeme na miundombinu mingine, wajue ni kodi za wananchi wenyewe ambazo wanailipia anapofanya ununuzi wa bidhaa mbalimbali.


Alisema serikali inafanya jitihada kubwa za usambazaji wa maji safi na salama lakini kuna baadhi ya maeneo ya kilimo hayajafikiwa na miundombinu hiyo, hivyo kuna haja ya kurejesha jambo hilo kwa wananchi wa kijiji hicho.

Waziri Saada aliitaka ZRA kuangalia namna ya kuendelea kusaidia maeneo mengine ambayo yanahitaji miundombinu hiyo.

"Wananchi wa Donge mtambue kuwa kisima hiki ni kodi zenu wenyewe ambazo zinamuwezesha mwananchi kudai risiti za kielektroniki hivyo tuendelee kulipa kodi kwa kudai risiti kila mnapofanya manunuzi," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya ZRA, Prof. Hamed Rashid Hikmany, aliwataka wananchi kuendelea kuisaidia serikali kupata mapato ili kumwezesha Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi aendelee kufanya maendeleo makubwa kwa kushajihishana kudai risiti za kielektroniki.

Pia aliwataka wafanyabiashara kuwapa risiti wananchi ili kuwa waaminifu na kodi inaifikia serikalini ili kutekeleza upatikanaji wa huduma mbalimbali muhimu kwa maslahi ya taifa.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA),Profesa Hemed Hikman (wapili kushoto) akiwa pamoja na Waziri wa Fedha, Dk Saada Mkuya wakimkabidhi kiti mwendo, Adam Suleiman Ali mwenye ulemavu wa viungo katika hafla ya ugawaji vitu kwa watu wenye ulemavu mkoa wa Kusini Unguja, hafla iliyofanyika kijiji cha Paje, Kusini Unguja ikiwa ni wiki ya shukrani kwa walipakodi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mkurugenzi avalia njuga uvuvi haramu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar, Dk. Salum Soud Hamed, amewataka wavuvi wa ghuba ya Chwaka kufuata sheria za uvuvi ili kuleta maendeleo kwa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira na rasilimali za Bahari.

Aliyasema hayo jana wakati wa kuangalia eneo litakalofaa kwa majaribio ya kutega nyavu katika maji ndani ili zisiathiri rasilimali za bahari katika ghuba hiyo.

Dk. Salum alisema amesikitishwa na kitendo cha wavuvi wa Chwaka kutotoa ushirikiano kwa taasisi za serikali ambazo zimefika kwa ajili yao na kusababisha kusita kwa kazi hiyo jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi za serikali.

'Hii ni moja ya utekelezaji wa azimio la Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, aliagiza yafanyike wakati wa kikao cha maridhiano kati ya wavuvi wa Chwaka na ghuba ya Chwaka kwa namna ya kuona nyavu zitavyofanya kazi katika ghuba hiyo," alisema.

Mtaalamu wa Mambo ya Bahari kutoka Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Haji Shomar, alisema ushirikiano wa pamoja yanahitajika kwa idara ya uvuvi na kamati za uvuvi za Chwaka kwa ajili ya kuzuia matumizi ya nyavu katika ghuba ya Chwaka.

"Kutokana na bahari yake ilivyo lazima wavuvi wakavue nje ya hifadhi za bahari ili kuepusha mgogoro wa wenyewe kwa wenyewe," alsiema mtaalamu huyo.

Ofisa Uvuvi wa Wilaya ya Kati Unguja, Ali Mwali Mahfoudh, alivitaka vikosi vya usalama kikiwamo Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) kuendelea kutoa ushirikiano juu ya ufanyaji wa doria katika hifadhi za bahari ili kupambana na uvuvi usiokubalika kisheria katika ghuba ya Chwaka.

Washiriki wa majaribio hayo wameiomba sereikali kudhibiti uvuvi wa nyavu katika ghuba ya Chwaka kutokana faida kubwa iliojitokeza juu ya kuzaliwa samaki kwa wingi katika maeneo yaliohifadhiwa ndani ya ghuba hiyo.

Adam Veso Ramadhani, mmoja wa washiriki hao kutoka Kijiji cha Uroa, aliwataka viongozi wanaowaunga mkono baadhi ya wavuvi wanaofanya uvuvi usiokubalika kisheria kuachana na tabia hiyo kutokana na faida ya kuhifadhi bahari inaonekana katika maeneo mbalimbali yaliohifadhiwa.

Katibu wa Wavuvi Shehia ya Marumbi, Haji Khamis Ali, aliomba serikali kufanya juhudi ya kuwadhibiti wavuvi ambao wanaendelea na uvuvi haramu katika shehia zao.

Vijiji sita kati ya saba vilivyomo ndani ya ghuba Chwaka, viko tayari kutoa ushirikiano kwa serikali katika kutii sheria bila shuruti isipokuwa kijiji cha Chwaka pekee.



OKEKE
UKURASA 14





# WAMENG'ANG'NIANA

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Zuchu, amesema mapito yake katika uhusiano wa kimapenzi na Diamond Platnumz, yameambatana na nyakati ngumu na furaha.

Akizungumzia maisha yake ya kimapenzi, Zuchu amesema wengi wanamuona kama mwanamke king'ang'anizi, lakini kamwe hawezi kufikiria kuachana na Diamond kwa sababu wote wanang'ang'aniana.

"Katika mapenzi kuna muda unakerwa kiasi ambacho unaapa huwezi kurudi kwake, lakini unarudi nyuma kutokana na maelezo yake (Diamond) na unamuonea huruma," amesema Zuchu.

Amesema wakati fulani anapopitia usumbufu mara nyingi huwa anawaza kuachana naye, lakini anaona hilo sio suluhisho kwa kuwa inapotokea jambo linamuhusu Diamond na yeye lazima atahusika kutokana na kuwa wapenzi.

Msanii huyo amesema kutokana na vitu vichache anavyokutana navyo, amejifunza mengi ikiwamo kuwa na usiri na kuchambua vitu vya kuweka mtandaoni.

"Natambua umuhimu wangu kwake, wale wanaosema king'ang'anizi, kwangu sikasiriki kwani raha ya kung'ang'ania nawe ung'ang'aniwe," amesema Zuchu.

BASI SAWA

## Dogo Sam akumbuka shule



RAPA anayekuja kwa kasi Sam One, amesema wakati umefika wa kurudi shule baada ya kushindwa kuendelea kutokana na kukosa pesa.

Akizungumza na EATV, Sam One, amesema umri wake bado unamuhitaji kuendelea na masomo huku akifanya muziki ambao umempatia mafanikio kwa kipindi kifupi.

Sam One ambaye anatamba na ngoma yake 'Msoto' amekuwa miongoni mwa wasanii wachache ambao wameonesha vipaji vyao vya muziki wakiwa na umri mdogo.

## Chino amkataa shetani



MKALI wa Amapiano, Chino Kidd, amesema anapiga pesa nyingi katika muziki licha ya kuonekana burudani sawa na ushetani.

Akizungumza hivi karibuni, Chino, amesema kupitia muziki amenunua magari na kujenga jumba la kifahari na kamwe haoni kama anafanya jambo la dhambi, kwa sababu shetani anapatikana kila mahali na sio muziki pekee.

Shetani anapatikana kila mahali, ukisema muziki sawa na ushetani unakosea kwani mimi nimefanikiwa kwa kupata pesa nyingi kwa bidii yangu na wala sio shetani. Ninavyojua shetani hakimbiwi unatakiwa kumshinda na kama huwezi kemea," amesema Chino.



# NANDY AFUNGA MWAKA AKIWA MWANZA

MWANAMUZIKI mkali wa Bongo Fleva, Nandy, amesema atamaliza mwaka na wakazi wa Mwanza kwa kutoa burudani ambayo itakumbukwa na kila mtu.

Nandy kupitia ukurasa wake wa Instagram, amesema kwa kuwajali mashabiki wa kanda ya ziwa, ameamua kutoa burudani katika jiji hilo kwa ajili ya kufurahia mwaka mpya  na mashabiki zake.

"Nitakuwa Mwanza usiku wa kuamkia mwaka mpya, nataka kuburudika na mashabiki zangu wakiwemo wazazi na watoto wao. Nataka tufurahi pamoja huku tukiukaribisha mwaka kwa pamoja," amesema Nandy.





# D Voice anazidi kuwakera

MSANII wa Bongo Fleva, D Voice ameeleza mwezi ujao atawaonesha baadhi ya wasanii namna gani ya kuthaminisha muziki kwa kutoa video yenye kila aina ya ubora.

D Voice na Zuchu ambao wote wanatoka lebo ya WCB, wapo mbioni kuachia video ya wimbo wao mpya 'Hujanizidi' ambao hadi sasa unaendelea kutamba katika majukwaa ya muziki.

Kupitia ujumbe aliouchapisha kwenye ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo amewataka mashabiki zake kuwa tayari kupokea zawadi hiyo ambayo hawajawahi kukutana nayo kwa wasanii wengine.

# MWAMBA HUYU, MIKA MWAMBA

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa muziki wa bongo fleva hapa nchini umekuwa ukitamba kimataifa. Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo muziki wa kizazi kipya umekuwa ukipendwa na kuheshimiwa sana nje ya mipaka yake.

Wasanii mbalimbali kwa sasa wamekuwa maarufu na wanapiga pesa ndefu kutokana na ngoma zao mbalimbali.

Mwanzo haikuwa rahisi. Muziki wa kizazi kipya ulionekana kuwa ni wa kihuni wakati unaanza kutanua mbawa zake mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kuna watu wanapaswa kupewa heshima zao kwa kuuondoa kuonekana kuwa ni wa kuhuni na kuufanya wa heshima kupendwa na hata watu wazima.

Joseph Mbilinyi maarufu kama Sugu na Joseph Haule, Profesa Jay ni moja kati ya wasanii wachache walioigeuza bongo fleva kutoka ilikotoka na kuwa hapa leo ilipo.

Hiyo ni kwa upande wa uimbaji, lakini pia wapo watu nyuma yao, wanaitwa maproduzya. Hawa ni watayarishaji wa muziki.

Ndiyo wanaowatafutia wasanii hao mirindimo kwenye nyimbo zao wanazotamba.

Wakati wa kupigania mapinduzi ya bongo fleva kukiwa na nyimbo za hip hop, R&B, zouk miaka hiyo, wapo maproduzya ambao nao walikuwa na mchango mkubwa kwenye kuifanya tasnia hiyo kukubalika.

**Mika Mwamba**

Jina lake kamili ni Miikka Aleksanteri Kari raia wa Finland. Wasanii na mashabiki wa muziki wanamtambua kama Mika Mwamba.

Anatajwa kuwa ndiye mtayarishaji muziki bora zaidi kwenye muziki wa kizazi kipya. Umaarufu wake ulikuwa mkubwa kuanzia miaka ya 2000, alipowatengenezea ngoma kali wasanii kama Dully Sykes, Inspector Haroun, Lady Jay Dee, Mad Ice, Chegge, Mandojo na Domo Kaya, Solid Ground Family, Complex, Zahrani (maarufu kama Big Punisher wa Bongo), Only Face, Dknob, Daz Nundaz na wengineo.

**P Funk**

Huyu ni mtayarishaji muziki na mmiliki wa Studio ya Bongo Records. Jina lake kamili ni  Paul Matthysse. Ni mmoja wa maproduzya waliowapandisha chati wasanii wengi kama Solo Thang, AY, Zay B, Mangwea, Sista P, Mike T, Ze Pungu, Jay Mo, Chege, Temba, na baadhi ya wasanii wa TMK, pia alishawahi kufanya kazi na Profesa Jay, Afande Sele, Ferouz. Wengine ni Mr II Sugu, Monduli Mobb, Gangwe Mobb, Hop Pot Family ikiongozwa na Soggy Doggy, na Manyema Family.

**Master J**

Anaitwa Joachim Kimario, maarufu kama Master J. Ni mtayarishaji aliyewekeza kwenye studio kadhaa tofauti, na moja ya sifa zake ni kwamba mbali na bongo fleva, lakini pia mtayarishaji wa muziki wa kwaya, pamoja na muziki wa dansi pia. Bendi nyingi za dansi kipindi hicho kama FM Academia, African Stars 'Twanga Pepeta', TOT Plus zilikuwa zikienda kurekodi kwenye studio zake, chini yake mwenyewe. Moja ya studio zake maarufu ni MJ Production.

**Henrico**

Ni mmoja wa watayarishaji maarufu wa muziki wa bongo fleva ambaye naye huwezi kumuacha kwenye orodha ya watayarishaji walioibeba tasnia ya muziki wa kizazi kipya, akifanya kazi na wasanii wengi nchini.

Henrico alikuwa kinara studio ya Soundcrafters.

**Said Comorien**

Wasanii wa zamani wa bongo fleva na mashabiki wake hawawezi kumsahau Said Comorien. Alikuwa mtayarishaji muziki alifanya kazi na wasanii mbalimbali, akiwemo Rehema Chalamila, maarufu kama Ray C na wengineo.

Metro Studio, ndiyo alikuwa akiimiliki.

FILAMU

# Mjomba si Mjomba

**Na Adam Fungamwango**

KUNA binadamu hapa duniani wanapenda sana utajiri kwa njia ya mkato. Yaani watapenda utajiri, lakini hawataki kuutolea jasho. Hao ni watu hatari kwa sababu wapo tayari kufanya kitu chochote ili mradi tu kutekeleza azma yake. Huyo yuko tayari kuutoa utu wake, kudharuliwa, kuchekwa, kunyanyaswa, na hata kutoa uhai wa mtu. Tena siyo mtu tu hivi hivi hata ndugu zake wa damu moja wakati mwingine hata wazazi wake.

Filamu ya 'Mjomba' inaakisi hiki ninachokiandika hapa.

Inaanza kuonesha maisha ya Sam na dada yake Davina. Waliishi maisha mazuri na mama yao ambaye alikuwa na uwezo mkubwa wa kiasi cha kuajiri wafanyakazi kwenye kampuni yake. Kifupi alikuwa tajiri.

Wanatembelewa na mjomba wao Suma ambaye anaongeza familia. Mama Sam anampeleka kaka yake kwenye kampuni yake akafanye kazi, lakini hataki kwa madai anafanyishwa kazi za udhalilishaji, ili hali yeye ni kaka wa tajiri kwenye kiwanda.

Dada yake anamwambia tatizo ni elimu yake ndogo, pia kutokuwa na ujuzi na uzoefu wa kitu chochote hapo.

Kuna siku ambayo familia nzima ilikwenda disko na kumuacha mama Sam nyumbani peke yake. Huku anavamiwa na majambazi na kuuawa. Kifo chake kinasikitisha watu wengi, na hakuna aliyekamatwa wala kushukiwa.

Siku isiyo na jina, Sam anamsikia mjomba wake Suma akiongea kwenye simu na watu walioonekana kuna pesa hajawamaliziwa, lakini maongezi yalionesha kuwa walifanya kazi ya kumuua mama yake.

Hasira aliyonayo anakwenda kumwambia mjomba wake kuwa ndiye aliyesababisha mama yake afe.

Utajiri wa ghafla unamjia Suma kwa sababu akawa kama ndiye mmiliki wa kampuni, badala yake Sam na dada yake Davina.

Suma alipoona Sam anaonekana kujua, akaagiza wauaji wake wale wakamuue Sam. Walipofika hawakumkuta yeye, bali dada yake Davina, wakamuua.

Hilo linamfanya Sam kutokuwa na la kufanya zaidi ya kulipiza kisasi. Akaanza kuua wote waliomuua mama yake na dada yake mmoja baada ya mwingine.

Suma, akaagiza wauaji wawili wa kukodi toka nje ya nchi. Hao ni Blade na Mr Karan. Wako fiti kweli kweli. Sam ambaye naye ni mjuzi wa sanaa wa mapigano, awali alipigwa. Lakini alikaa imara na kurejea tena na kuanza kupiga wote na kuwaua, mwisho makampuni na mali zote na nyumba zikarudi mikononi mwake.







# Mwendo wa paka wamponza Burna Boy

MSANII nyota wa Afrobeats kutoka Nigeria Burna Boy, amewajibu watu wanaomshutumu kwa kutembea kike jukwaani, akisema hawezi kulumbana nao kwa sababu ana mambo mengi ya kufanya.

Hivi karibuni video ilisambaa inayomuonesha mwanamuziki huyo akitembea jukwaani kama mwanamke na kuibua mjadala mkali, huku wengi wakijiuliza imekuwaje.

"Wanapozungumza hakuna anayejali, lakini ninapojibu inakuwa kama maafa ya Nyuklia. Sijui ni kitu gani, lakini nina mengi ya kupoteza sasa, Walahi wengi wenu hamngekuwa hapa tena, wacha niende kununua kitu kingine nikapumzike." ameandika Burna Boy.



## AY Makun ajipa moyo

MCHEKESHAJI na mtayarishaji filamu kutoka Nigeria, AY Makun, amesema wanaume hawamuungi mkono katika kazi yake jambo ambalo linamuumiza sana.

AY aliandika kupitia ukurasa wake wa X, kwamba anachotambua ipo siku moja wataona nguvu yake kwa sababu kufanya kazi kwa bidii kutasalia kuwa muhimu katika jamii.


"Mimi bado ni mwanamume pekee niliyesalia kwenye biashara ya utayarishaji filamu ambaye bado sijakata tamaa. Binafsi nitaendelea kuisukuma kwa kifua changu," ameandika AY.

## Okeke alianzisha kiaina

KATIKA hali isiyotarajiwa, mwigizaji wa Nollywood Gideon Okeke amemwelezea msanii mwenzake Jim Iyke, kuwa sawa na mtoto katika tasnia ya sanaa.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, mwigizaji huyo alimshutumu Iyke kwa kukosa taaluma na tabia isiyofaa wakati akitoa maoni kuhusu usalama wa mahali pa kazi ndani ya tasnia ya filamu nchini Nigeria.

"Nimekutana na watu wengi, pia hata Jim Iyke ambaye anataka kuwa samaki wa dhahabu, lakini hana tabia ya mvulana, mimi kwangu sawa na mtoto tu," ameandika Okeke.





## Kanayo awananga wanawake wazee

MWIGIZAJI maarufu wa Nigeria, Kanayo O Kanayo, amewatahadharisha wanawake wenye umri wa miaka 30 kuishi bila mume, akisema wanahitaji maombi ya dharula.

Mkongwe huyo wa Nollywood, alishiriki maoni yake kwenye kipindi cha Soni Irabor Live, akieleza wanawake kama hao walikataa maendeleo ya wenzao wa kiume walipokuwa na umri wa miaka 18 hadi 20.

"Msichana atakuwa chuo kikuu akiwa na miaka 18 hadi 20, hapo anaanza kupata wanaume na nyakati fulani mzee sana. Halafu, unachokiona anakataa kuwa nao na umri unapokwenda anakuwa hana la kufanya na hapo ndipo anahitaji maombi ya dharula," amesema.

## Wizkid aibua utata mwingine

IMEKUWA vigumu kueleweka, lakini kwa mwanamuziki wa Nigeria, Wizkid, ameamua kujitoa hadharani na kueleza anampenda msanii mwenzake Olommide.

Tangazo hilo ambalo limewashangaza mashabiki wengi wa muziki, limeibua maswali mengi kuhusu kuelewana kwa wanamuziki hao ambao kila wakati wanakuwa kwenye ugomvi.

Kupitia ukurasa wake wa X, mwimbaji huyo wa ngoma ya Kese' alimtaja Olamide Adedeji, anayejulikana zaidi kama Olamide, kuwa rafiki na ana mapenzi naye kila siku.



# Vijana 1,000 wapigiwa chapuo mikopo halmashauri

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

ZAIDI ya vijana 1,000 wenye ndoto za kuendesha biashara za kidijitali katika mkoa wa Arusha, wamepigiwa chapuo na serikali kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri bila riba, baada ya kulegezwa masharti.

Julai Mosi, mwaka huu, serikali ilianza kutoa tena fedha za mikopo hiyo nchini baada ya kusitishwa Bungeni, Dodoma Aprili 13, 2023.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Arusha, Richard Mwihechi, amewataka vijana hao kuzipa mgongo changamoto zinazotokana na mikopo ya kausha damu na badala yake, kuchangamkia fursa hiyo ili kuendeleza biashara zao na kukua kiuchumi, badala ya kulalamika kukosa ajira mitandaoni.

Mwihechi aliwahamasisha vijana hao jana wakati akifunga mafunzo ya miezi miwili yaliyoendeshwa na mashirika matatu ya kiraia ya Her Initiative, Master Card Foundation na DoT.

"Kwa sasa kikundi cha watu watano kila mmoja anaweza kuchukua mkopo kulingana na mradi alionao kijana, tofauti na kipindi cha nyuma ilikuwa ni mradi wa kikundi ndio ulikuwa unaangaliwa.

**"Kwa sasa kikundi cha watu watano kila mmoja anaweza kuchukua mkopo kulingana na mradi alionao kijana, tofauti na kipindi cha nyuma ilikuwa ni mradi wa kikundi ndio ulikuwa unaangaliwa.**

"Lakini pia hata umri wa kijana anayekopeshwa kwa sasa ni kuanzia miaka 18 hadi 45, wakati kipindi cha nyuma ilikuwa kuanzia miaka 18 hadi 35. Hivyo ninatoa rai kwa vijana kuchangamkia fursa hii ya mikopo," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Tanzania Project, ambayo ni miongoni mwa taasisi za kutoa elimu hiyo, Baraka Joel, alisema vijana hao wamepata muda wa kujifunza zaidi juu ya kukuza na kuendesha biashara kidijitali.

"Kwa takwimu za nchi yetu, zaidi ya asilimia 65 ya watu ni vijana. Tumeona tuwasaidie kujifunza mbinu mbalimbali za kukuza biashara zao, hasa katika dunia ya sasa ya sayansi na teknolojia. Sisi kama Tanzania Project, tumeweza kuwasaidia vijana 50, tunaamini kuwa maisha yao yatabadilika kiuchumi," alisema Joel.

Aidha, mashirika hayo yanalenga kuwafikia vijana 1,500 kwa mwaka 2024 /2025, kwa kuwapa elimu ya kuendesha biashara kidijitali katika kuufikia uchumi wa kati.

# Ujenzi madaraja yaliyoharibiwa na El - nino waanza

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

UJENZI wa madaraja matano yaliyokuwa yameharibiwa vibaya na mvua ya El-Nino mkoani Manyara mwaka jana, umeanza hatua za awali za utekelezaji wa mradi huo, baada ya serikali kuidhinisha zaidi ya Sh. bilioni 17 za dharura kwa ajili hiyo.

Fedha hizo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia (WB), uliochukuliwa na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS).

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Matengenezo wa TANROADS mkoani Manyara, Greyson Ndyamukama, fedha hizo ni kati ya zile zilizoombwa na serikali kutekeleza mradi wa ujenzi wa madaraja 13 nchini yenye thamani ya Sh. bilioni 62.

Ndyamukama alisema kutokana na ufinyu wa bajeti ya matengenezo ya kawaida, muda maalum na madaraja makubwa serikali iliomba mkopo wa kutengeneza miradi ya dharura iliyoharibiwa na mvua ya El-Nino kutoka Benki ya Dunia ili kusaidia kutengeneza madaraja.

Mkuu huyo aliyataja madaraja hayo kuwa ni Daraja la Minjingu, ambalo mkataba wake umewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki, wakati Daraja la Losinyai/Njoro, wako kwenye makubaliano.

Madaraja mengine ni la Katesh ambalo mkataba wake ulitiwa saini Novemba Mosi, mwaka huu, daraja dogo eneo la Dabir la Dareda/Dongobesh ambalo mkataba wake umeshatiwa saini na daraja dogo la Msasani, mkataba umeshatiwa Saini pia.

Aidha, Ndamukama alisema kwa mwaka wa fedha 2024/25 serikali iliwaidhinishia Sh. bilioni 11 kwa ajili ya kutengeneza barabara kwa muda maalum, sehemu korofi na madaraja 83 na mpaka Septemba, mwaka huu, walifikia asilimia 95.

Alizitaja baadhi ya kazi walizofanya kuwa ni kuweka taa za barabarani, kuweka lami sehemu zilizoharibika, kusafisha mifereji na makalvati, kupanda miti na kufyeka majani na ujenzi wa Daraja la Langay.



Seif Hamad Kiputo mkazi wa Muheza mkoani Tanga (Kulia) akikabidhi zawadi za soda na maji kwa ajili ya sikukuu ya Krismas na Mwaka mpya kwa wakazi makundi mbalimbali juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mchungaji: viongozi kanisa wamejigeuza kuwa trafiki ibadani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Jimbo la Kilimanjaro Mashariki la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, Mchungaji Calvin Koola, amesema kuna viongozi wa kanisa wamejigeuza kuwa trafiki ibadani, wakati wa huduma ya matoleo.

Kutokana na kutopendezwa na ujanja huo wa baadhi ya viongozi wa kanisa, alisema jukumu lao si kukwepa kutoa sadaka kama wengine, bali ni kusimamia matoleo.

Mch. Koola alikuwa akizungumza katika Usharika wa Mwika, wakati wa mkutano mkuu wa tatu wa usharika huo unaoongozwa na Mchungaji Godlisten Terry.

Alisema viongozi hao wanachopaswa kukifanya, ni kuwa mfano mwema wa kumtumikia Mungu, wakati wa matoleo ya sadaka, kwa kuwa hivi sasa wako ambao hawatoi sadaka.

Katika mafundisho yake, aliwakemea viongozi mbalimbali katika sharika, ambao siyo mfano mwema wa utoaji kwani wao huwa kama 'matrafiki ibadani', ambao kazi yao ni kuwaelekeza washarika kupita huku au kule wakati wa matoleo.

"Wao wenyewe hawatoi sadaka. Ni muhimu wazee wa usharika wawe mfano mwema wa kumtumikia Mungu kwa sadaka. Isivyo bahati, wale wanaomtumikia Mungu kwa uaminifu hukumbana na vipingamizi vingi kutoka kwa kina Sambalati na Thobia; ambao wamejaa dharau na kubeza kazi inayofanywa na wale waliojitoa kwa dhati kumtegemea na kumtumikia Mungu.

"Ni muhimu usharika unapoweka mipango ya maendeleo na kuazimia kuitekeleza katika mkutano mkuu, washarika wasikatishwe tamaa kwa maneno ya dharau na kebehi kama vile hata hiki wanachokijenga, mbwa akipanda ataangusha ukuta.

"Washarika watiwe moyo kwamba, hata kama ni wanyonge, kujaribu ni bora kuliko kutokujaribu au kukata tamaa. Ni lazima tufanye uamuzi kwamba, kazi hii tuliyopewa na Mungu itafanyika. Niwatahadharishe wajumbe wa mkutano mkuu wasiwe ni watu wa kulala katika vikao na kisha kukurupuka na kusema ipite," alisema.

Akiwasilisha Mpango Mkakati wa Dayosisi ya Kaskazini ya KKKT wa mwaka 2024- 2028, Mratibu wa Makavazi ya Dayosisi hiyo, Mch. Enock Makundi, alisema mkutano huo mkuu wa tatu wa usharika, unapaswa kuazimia kuwa na mpango kazi wa usharika unaojielekeza katika mpango mkakati huo wenye vipaumbele vitano.

TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kasongo mbona wewo!!

## -Wimbo wa mwaka 1980, 'unaotrendi' kama utani 2024

**Na Adam Fungamwango**

KASONGO yeye, mombali nagai, Kasongo mbona wewo, songa libala, Kasonge yeye, yeye, Kasongo mbona wewo, mbona wewoo, mombali nanga yeye."

Hiki ni kionjo maarufu zaidi kwenye mitandao ya kijamii , wakati watu wakionesha vibonzo na kutaniana hasa kwenye mambo ya soka.

Haijulikana ni kwa nini kipande hiki kimechaguliwa na watu wengi kuhusishwa kwenye vibonzo, lakini mara ya kwanza kilianza kuonekana kikiimbwa na mchungaji kutoka Uganda, Aloysius Bujingo wa kanisa la 'House of Prayer Ministries' lililopo Makerere kuuimba wimbo huo mbele ya waumini wake.

Kipande cha video ile ambacho alikuwa akiimba, ndicho kimekuwa maarufu zaidi kwenye mitandao ya kijamii, facebook, X, instagram na tik-tok, huwezi kuingia bila kukutana na vibonzo au vichekesho.

Inawezekana kabisa huenda kipande cha wimbo huu kimekuwa maarufu mara baada ya kuchukuliwa na kuingizwa kwenye masuala ya soka.

Pamoja na kwamba kilikuwepo kwenye kichekesho na vibonzo, lakini kilipata umaarufu mkubwa na wa ghafla kilipoingizwa kwenye utani wa soka.

Ilianza Novemba 7 mwaka huu, Yanga ilipofungwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Mara baada ya mechi hiyo iliyokuwa na kipigo cha ajabu, ambapo si mara nyingi kwa timu kubwa kama Simba na Yanga kufungwa idadi kubwa ya mabao, lakini pia ilitoka kufungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, Novemba Mosi kwenye uwanja huo huo, mashabiki wa Tabora United na wa Simba waliungana kuwananga wale wa Yanga.

Video za kuwananga Yanga ziliambatana na sauti za mchungaji Bujingo iliyokuwa kwenye video aliyokuwa akiimba wimbo huo wa Kasongo.

Kila 'klipu' iliyokuwa inaitania Yanga ilikuwa na kibwagizo hicho, ndipo kilichopata umaarufu mkubwa.

Hata hivyo wengi bado hawajui asili ya wimbo huo, umetoka wapi, umeimbwa na bendi gani na je una maneno yanayofanana na hicho kipande yanayokuwa kwenye utani?

**WIMBO KASONGO UMETOKA WAPI?**

Huwezi kuuzungumzia wimbo huu kabla ya kuizungumzia bendi yenyewe iliyoupiga. Wimbo 'Kasongo' ulipigwa na bendi ya Super Mazembe iliyoundwa mwaka 1967 nchini Zaire, sasa (DRC) na kuongozwa na Longwa Didos Mutonkole, baadaye ilikwenda nchini Zambia, ambako ilikaa kwa muda na kumpata mwanamuziki,Nashil Pichen, ambaye aliamua kuwachukua na kuamua kuwapeleka jijini Nairobi nchini Kenya na kuweka makazi yake ya kudumu.

Baadaye pia ilibadilisha jina na kujiita, Super Mazembe likiwa na wanamuziki maarufu na nyota kama kina Lovy Longomba, Kasongo wa Kanema, Bukassa Bukalos, Atia Djo, Fataki Lokassa 'Masumbuko wa Dunia', Rondo Kandolo, Charles Atei, Lobe Namapako, and Loboko Pasi na wengine wengi.

Walifyatua nyimbo nyingi zikiwemo 'Kasongo', 'Atia Djo', 'Lovy', 'Gina', 'Loboko', 'Auma', 'Muana Nyau', 'Longwa', 'Samba', 'Lukasi', 'Ouma', 'Okova' 'Mulekeni Marry' na zingine nyingi.

Wimbo wa 'Kasongo' ulifanyuliwa mwaka 1980, ulitungwa na Katele Aley, huku kilichokuwa kiliimbwa ni kikiwa na maana tofauti na vibonzo zinavyoendelea mitandaoni.

"Kasongo yeye, mobali na ngai, Kasongo ngana weo, zonga libala ee..." Haya ni maneno halisi ya kilingala yaliyokuwa akiimbwa kwenye wimbo huo. Ukisoma nakuangalia vizuri hapa utagundua kuna utofauti wa matamshi au mashairi haya na yale pale juu ambapo alikuwa akiimba mchungaji kwani ilionekana hakuyaelewa au kuyatamka vyema maneno ya lugha hiyo maarufu nchini DRC.

Maana yake tafsiri ya kiswahili ya wimbo huo, ni kwamba mwanamke anamsihi mumewe Kasongo arejee nyumbani. "Kasongo mume wangu rudi nyumbani, Kasongo mimi na wewe, rudi nyumbani ee." Ni mke aliyechoshwa upweke, mumewe akiwa ameondoka nyumbani na kumuacha akiteseka na watoto na watoto akiwa hajulikani kama yupo nyumba ndogo au la. Hapo utaona kuwa maana ya wimbo huo, tofauti na hiki kinachoendelea cha kutoana 'akili' na kutaniana kwenye mitandao ya kijamii.







**Tuma meseji 0716 350534**

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Vurugu zaenea Msumbiji, polisi watano wauawa

**MAPUTO,** MSUMBIJI

HALI ya usalama inazidi kuwa mbaya nchini Msumbiji baada ya waandamanaji kuwaua polisi watano katika mji wa Namapa kwenye jimbo la Nampula.

Kwa mujibu wa tovuti ya Integrity Magazine, ilimnukuu mkuu wa polisi wa mji huo, akisema miongoni mwa polisi waliouawa ni mkuu wa operesheni ambaye alikuwa amehamishiwa eneo hilo kutoka mji mkuu wa Maputo.

Mkazi mmoja aliliambia Jarida la Integrity Magazine kwamba kiwango cha vurugu kiliwalazimu watu wengi kukimbilia vichakani kwa hofu, huku magari yakizuiwa na kusababisha msongamano barabarani.

Vurugu hizo zilizuia usafiri wa kutoka na kuingia katika jimbo la Cabo Delgado na jiji la Nampula.

"Hali ni ya wasiwasi hapa. Wanajeshi na polisi pia walikimbia," alisema mkazi mwingine wa Nampula.

Takriban watu 200 wanahofiwa kuuawa tangu kuanza kwa maandamano hayo ya kupinga matokeo ya uchaguzi Oktoba 21, mwaka huu.

Katika uchaguzi huo, mgombea wa chama tawala cha Frelimo, Daniel Chapo alitangazwa kuwa rais mteule baada ya kupata asilimia 65 ya kura zote zilizopigwa.

**BBC**

# Makamu wa Rais Korea Kusini naye afukuzwa

**SEOUL,** KOREA KUSINI

WABUNGE wa Korea Kusini, jana wamepiga kura ya kumng'oa madarakani Kaimu rais Han Duck-soo, wakimtuhumu kushiriki kikamilifu katika uasi baada ya aliyekuwa rais Yoon Suk-yeol, kujaribu kutangaza sheria za kijeshi Desemba 3, mwaka huu.

Kutimuliwa kwake kunakuja wiki mbili baada ya Rais Yoon Suk, naye kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye na sasa inasubiriwa Mahakama ya juu kuthibitisha au kukataa.

Hali hiyo ambayo imetajwa haijawahi kutokea Korea Kusini rais na waziri wake mkuu ambaye alikaimu nafasi hiyo kuondolewa madarakani na wabunge.

Wabunge walimng'oa Han Duck-soo kwa kura 192.

Pamoja na ukubwa wa tukio hilo, hali bado ni shwari ndani ya Bunge, huku maandamano ya umma yanapangwa kufanyika mbele ya majengo ya Mahakama ya Katiba, kushinikiza kukubaliana na kura za wabunge.

# Mkuu wa WHO anusurika katika shambulizi la anga

**SANAA,** YEMEN

MKUU wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na wafanyakazi wengine wa Umoja wa Mataifa, wamenusurika katika shambulizi la anga lililotekelezwa na Israel katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Yemen.

Shambulizi hilo lilitokea juzi katika uwanja wa ndege wa kimataifa ulioko katika mji mkuu wa Sanaa na kusababisha vifo vya watu watatu na majeruhi kadhaa.

Katika chapisho la mtandao wa kijamii, Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Adhanom Ghebreyesus, alisema yeye na wafanyakazi walikuwa karibu kupanda ndege wakati uwanja wa ndege ulipopigwa na mabomu kutoka angani.

"Mmoja wa wafanyakazi wa ndege yetu alijeruhiwa," aliandika na kuongeza kuwa watu wawili katika uwanja wa ndege waliuawa.

Mashambulizi hayo ambayo pia yamelenga vituo vya umeme na bandari, yamesababisha vifo vya watu watatu huku idadi kadhaa wakijeruhiwa.

Kundi la waasi la Houthi linaloungwa mkono na Iran limetaja mashambulizi hayo kuwa ya kinyama baada ya Israel kudai kuhusika.

Haijabainika iwapo waliouawa ni raia au waasi wa Houthi. Katika taarifa, Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), lilisema ndege zake za kivita zilifanya mashambulizi ya kijasusi kwenye kambi za kijeshi za utawala wa Houthi kwenye pwani ya magharibi na ndani ya Yemen.

Shambulizi hilo lililenga miundombinu ya kijeshi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Sanaa na vituo vya umeme vya Hezyaz na Ras Kanatib.

Pia bandari za Al-Hudaydah, Salif na Ras Kanatib kwenye pwani ya magharibi pia zililengwa.

Katika kauli yake muda mfupi baada ya shambulio hilo, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alisema nchi yake itaendelea kukata mkono wa kigaidi wa mhimili wa uovu wa Iran hadi watakapomaliza kazi.

Mohammed Ali al-Houthi, mkuu wa kamati kuu ya mapinduzi ya Houthis, aliita mashambulizi hayo kuwa ya kinyama na uchokozi.

**BBC**



Polisi wakimsaidia mhamiaji mmoja baada ya kuokolewa baharini akijaribu yeye na wenzake kuvuka kwa kutumia boti ndogo kwenda Ulaya kutafuta maisha bora.**PICHA: ALLIANCE**

# Watu 29 hawajulikani waliko wakidaiwa kutekwa Kenya

**NAIROBI,** KENYA

TUME ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu nchini Kenya (KNCHR), imesema watu 29 hawajulikani walipo baada ya kupotea wakati wa maandamano ya kuipinga serikali mwezi Juni mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa juzi, KNCHR ilisema imeona hali inazidi kuwa ya wasiwasi kutokana na vitendo vya utekaji watu unaoendelea kwa siri unaofanywa na watu wenye silaha wasiojulikana.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa tume hiyo pia ilibaini watu wote waliotekwa nyara wamekuwa wakipinga vikali serikali kwenye mitandao ya kijamii.

Inasema hadi sasa kuna visa vingine 13 vya utekaji nyara au kutoweka kwa watu katika muda wa miezi mitatu iliyopita na kufikisha jumla ya kesi 82 kuanzia Juni.

"Kesi saba za utekaji nyara za hivi karibuni ziliripotiwa mwezi huu, huku sita kati yao wakiwa bado hawajulikani waliko, na hivyo kufanya jumla ya watu 29 ambao hawajapatikana tangu Juni 2024," ilisema taarifa hiyo. Tume hiyo ilisema kuwa utekaji nyara huo unafanyika kinyume na katiba na unapaswa kushughulikiwa haraka.

"Tume inatahadharisha kwamba ikiwa tabia hizi za utekaji nyara zitaendelea, basi tutakuwa tunarudi kwa kasi katika siku za giza za historia yetu ambapo mashambulizi hayo yalikuwa yanaleta hofu kwa mtu yeyote anayeikosoa Serikali," ilisema.

KNCHR pia ilipinga taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi la Kenya, IGP Douglas Kanja, ambaye alikanusha polisi kuhusika na utekaji nyara wa watu.

Tume hiyo ilisema jeshi la polisi linapaswa kuendelea kuwa makini katika kutekeleza majukumu yao ya kulinda raia, na kuongeza kuwa watu wanatakiwa kukamatwa kulingana na sheria.

Ilisema matukio hayo yanafanyika mchana kweupe, huku baadhi yao yakinaswa na CCTV.

**BBC**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Mabasi yaliyokuwa maarufu zamani hivi sasa yamebadili safari zake na kutoa huduma ya kwenda vijijini. Pichani yakiwa yameegeshwa eneo la stendi ya Mlandege mjini Iringa yakisubiri abiria wa kwenda vijiji mbali mbali vya mkoa wa Iringa jana **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Mkufunzi kutoka Shirika la Help Age, John Eddy akiongoza mdahalo kwa makundi rika kata ya Mwamalasa wilayani Kishapu kujadili hali ya matukio ya ukatili wa kijinsia na kutafuta ufumbuzi wake ili kuyapunguza. **PICHA:MARCO MADUHU**



Wazee wasiojiweza wanaoishi katika kituo cha Mother Tereza kilichopo Hombolo jiji la Dodoma wakishiriki kula chakula cha pamoja katika Sikukuu ya Krismasi kilichotolewa na watumishi wa kampuni ya JUMACO inayojishughulisha na upimaji ,uuzaji wa viwanja na uchoraji ramani za majengo. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Moja ya madarasa ya Shule ya Sekondari Muoji iliyopo kijiji cha Muoji, jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, sekondari hiyo inatarajiwa kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari mwakani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# HADITHI

# Malaika shetani-1

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumuona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumuangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo hukupata kudhani. Unawezi kukutana na mtu ambaye kwa muonekano na jinsi anavyokutendea ukamuona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana. Kwenye kijiji kimoja kilichopo Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini. Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa. Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wanakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Haikuwa siku nzuri kwa wanakijiji wa Mikamba, Bungu Rufiji. Ni baada ya mwanafunzi wa kidato cha tatu katika shule ya sekondari Kikamba kuuawa. Anaitwa Naima. Mmoja wa wasichana warembo kijijini hapo. Japo alikuwa mwanafunzi alikuwa na sura nzuri, pamoja na umbo ambalo lilimtamanisha mwanaume yeyote atakayekutana naye njiani.


Uwe kijana au mzee, utageuka na kumuangalia msichana huyo kwa jicho la ushawishi.

Nyumbani kwa wazazi wake hakukuisha wageni. Kutoka kijiji hicho cha Mikamba na vingine jirani. Wote walikuja na nia moja ya kuleta barua ya kutaka kumuoa. Kila barua ilipigwa chini. Yeye mwenyewe pamoja na wazazi wake hawakuwa tayari. Wazazi wake walitaka mtoto wao asome kwani waliona ana akili sana darasani na mara kwa mara alikuwa akishika nafasi ya kwanza, hivyo waliona anaweza si kuwasaidia wao tu kama wazazi, pia kulisaidia taifa.

Hawakuwa kwenye hali nzuri kimaisha, lakini walijiweza kutokana na kuwa na mashamba ya mazao ya biashara na mengine ya chakula. Mzee Bakari, baba yake Naima alikuwa pia na mifugo ambayo ilimsaidia sana kumsomesha mtoto wake. Aliuza kuku, ng'ombe na hata maziwa kwa ajili ya kupata ada ya kumsomesha Naima. Binti alisomesheka pia. Hakutaka upuuzi. Licha ya uzuri wake ambao ulimfanya apate usumbufu kila anapokwenda, kila anapopita, haikumundolea lengo la kutaka kusoma na baadaye kuwa daktari. Alipenda sana watoto. Alitaka kuwa daktari wa watoto. Alisumbuka na kujiuliza sana ni kwa nini huwa wanalia sana. Na wanapolia huwa wanajisikia nini? Huwaza kama mkubwa anaweza kusema kichwa, tumbo au mkono unauma, lakini mtoto mchanga hawezi kusema chochote. Analia tu mpaka pale mama yake atakapobaini mwenyewe kitu gani kinamsumbua. Hiyo ilisababisha awaonee huruma sana. Akaamua kusoma kwa bidii na kuacha upuuzi wote. Leo hii ndoto yake imekatishwa. Imekatishwa kwa kuuawa. Ndiyo ameuawa kwa mujibu wa wanakijiji cha Mikamba.

Mwili wake umekutwa kwenye pori la kijiji hicho, ukiwa umepigwa vibaya na umezikwa nusu. Yaani kuna upande ulikuwa umefukiwa na upande mwingine haukufukiwa.

Wauaji walifanikiwa kumuua, lakini hawakufanikiwa kumfukia. Lengo inaonekana ni kumuua na kumfukia.




**"Naima mwenye uzuri wa kuvutia, sura ya kupendeza, mwili laini, ngozi kama sufi, leo hii mwili wako unalala kwenye udongo?" Alisikika akisema kijana mmoja ambaye haikujulikana alikuwa anauliza au anaomboleza baada ya kuona mwili wa Naima unashushwa kaburini.**

Kumfukia kwao ilikuwa ni kuua ushahidi. Wangefanikiwa ina maana Naima ingesemekana amepotea. Ametoweka, hivyo ingewapa kazi wanakijiji kumsaka huku na huko bila mafanikio. Hawakufanya hivyo. Inaonekana si kwa bahati mbaya. Kuna kitu ambacho kimesababisha kutimiza lengo lao muhimu kabisa la kupoteza ushahidi. Kwa wauaji, kutoa roho ya mtu ni jambo dogo sana. Kazi kubwa inabaki kupoteza ushahidi ili wanaofuatilia, iwe wananchi, raia au askari polisi wakianza upelelezi wao washindwe kupata chochote kitakachowapeleka mbele ya sheria wauaji. Inaonekana ni kama walikimbia. Inawezekana kulikuwa na mtu anapita eneo la tukio muda ambao wanaanza kumfukia, ndipo waliamua kukimbia. Hata hivyo wapo wanaojiuliza, ni kwa nini alipopita hawakurudi kuendelea na kazi yao? Wengine wanajiuliza wauaji waliokuwa na roho ya kikatili kumuua Naima kwa nini wakawa na roho nzuri kutomuua yule ambaye aliwakuta wanamfukia? Hizo zote ni dhana, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa Naima ameuawa.

Wanakijiji walikuwa wamekusanyika nyumbani kwa wazazi wa marehemu. Kila mmoja alikuwa na huzuni. Binti mwanafunzi, mrembo na mbichi kama yule kuuawa. Wengi walikuwa wanahusisha na mambo ya mahusiano. Walijua urembo kama ule aliokuwa nao ni lazima alikuwa na mpenzi wake ambaye labda amemuua kutokana na masuala ya wivu. Hata hivyo wengi wanakiri kuwa hawajawahi kumuona mpenzi wa Naima. Alikuwa ni msichana anayecheka na watu wote, wanaume na wanawake, vijana kwa wazee, lakini hawakuwa na ushahidi wowote kuwa alikuwa na mahusiano na mwanaume fulani. Hii nayo iliwachanganya wengi. Ndani ya nyumba kulisikika vilio kutoka kwa ndugu, familia, jamaa na marafiki. Viongozi wa kijiji, kata na mkoa walifika hapo nao kujumuika na wanafamilia kutokana na msiba mzito.

Mzee Bakari hakulia, lakini alionekana mwenye huzuni kubwa. "Nimepotelewa na mtoto ambaye nilikuwa namtegemea. Yeye ndiye tegemeo la familia nzima. Nimefanya kila kitu kwa ajili yake, leo hii kila kitu kimefutika ghafla kama mwalimu anavyofuta maandishi ubaoni. Kwa hili nataka haki itendeke. Najua chochote kile kitakachofanyika hakitawezesha binti yangu kurudi duniani, lakini nataka yeyote aliyehusika awajibike na hili," alisema kwa namna ya kuomboleza mzee Bakari.

Kitu ambacho ndugu wengi walichoshukuru ni kupatikana kwa mwili wa Naima, angalau uzikwe kwaa heshima kama binadamu tofauti na kama ungefukiwa na wauaji.

Muda wa kwenda mazikoni ukawadia na watu wengi walishiriki mazishi ya binti huyo, kila mmoja akimtukuza mwenyezi Mungu.

"Hata binti mzuri na mrembo kama huyo anakufa, kweli kifo ni fumbo, kifo ni kwa kila mtu, haijalishi mzuri na mbaya, masikini na tajiri," alisikika mama mmoja mtu mzima.

"Naima mwenye uzuri wa kuvutia, sura ya kupendeza, mwili laini, ngozi kama sufi, leo hii mwili wako unalala kwenye udongo?" Alisikika akisema kijana mmoja ambaye haikujulikana alikuwa anauliza au anaomboleza baada ya kuona mwili wa Naima unashushwa kaburini.

Baada ya maneno hayo alionekana kushindwa kujizuia, akaangua kilio. Rafiki zake wakamshika na kumpeleka pembeni kidogo huku wakimbembeleza.

Kijana huyo alikuwa mmoja wa vijana wengi waliojaribu kumtaka Naima kimapenzi. Lakini aligonga mwamba. Pamoja na kugonga mwamba aliendelea kuheshimu hisia za msichana huyo, pia aliendelea kumpenda na kila anapomuona moyo wake hulipuka. Naima alikuwa akiwaambia wote wanaomtaka kuwa yeye bado mwanafunzi, bado mdogo na hawezi kujiingia kwenye masuala ya mahusiano kwani ana ndoto zake kwenye maisha yake ya baadaye. Yeyote anayemtaka kweli amsubiri mpaka pale atakapotimiza ndoto zake atakapomaliza kusomea udaktari.

Hii ilisababisha vijana wengine na hata baadhi ya watu wazima kumchukia, lakini wapo waliokubaliana na anachokitaka mwenyewe na waliendelea kushirikiana naye.

Kwa bahati nzuri alikuwa ni msichana mcheshi mwenye heshima kwa kila mtu. Hicho kilisababisha hata wale waliomchukia kwa sababu tu ya kukataliwa kuendelea kumpenda. Labda kwa kudhani ipo siku atabadili mawazo yake.

**Itaendelea Jumamosi**

# PRISONS YATAMBA IMEANZA LIGI, MINZIRO AWAPONGEZA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Pamba Jiji katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya, Kocha Msaidizi Prisons, Shaaban Mtupa, amesema huo ni mwanzo wa matokeo mazuri ambayo watayapata katika michezo ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Ulikuwa ni ushindi wa kwanza kwa Prisons baada ya kucheza michezo mitano, mara ya mwisho kuvuna pointi tatu ilikuwa Novemba 3, mwaka huu walipoifunga KenGold bao 1-0.

Mtupa, mshambuliaji wa zamani wa timu hiyo ametamba kwa sasa wao ndio wameanza ligi.

Kocha huyo alisema kwa kiasi kikubwa wamefanyia kazi mapungufu yaliyokuwa katika kikosi chake hasa kwenye safu ya ulinzi na ushambuliaji.

"Tulihitaji sana pointi tatu, na kweli hatimaye tumezipata, lakini haikuwa mechi rahisi, wachezaji wa pande zote mbili walionekana kucheza kwa wasiwasi, unajua hizi timu zote tumekuwa na shida ya kupata ushindi katika ligi, na hatupo maeneo salama kwenye msimamo.

Nilichokuwa naangalia sana katika mazoezi kabla ya mechi hii ni eneo langu la ulinzi na ushambuliaji, nimefanikiwa kwa kiasi fulani kulirekebisha, niwapongeze sana vijana wangu wamepambana, kila mtu kajitoa mpaka kupata ushindi huu," alisema Mtupa.

Aliongeza kama hali itaenda kama alivyoirekebisha na kupata wachezaji wa kuongezea kipindi cha dirisha dogo la usajili, ana ukakika wa kufanya vyema katika mzunguko wa pili ambao wameuanza.

"Sisi kwetu ndiyo kwanza tumeanza ligi, tunatarajia kufanya vyema zaidi ya hivi," Mtupa alisisitiza.

Naye Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Fred Minziro, aliwapongeza wapinzani wake akisema walistahili kupata ushindi huo kutokana na wachezaji wao kupambana.

"Nawapongeza sana Prisons kwa sababu wamejitoa, wachezaji wao wamepambana sana, walistahili ushindi. Kwa upande wetu tumecheza vyema, lakini hatukuwa bora katika pasi za mwisho ili kufunga mabao," alisema Minziro.

Kwa sasa Pamba Jiji yenye pointi 12 ipo katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imecheza michezo 16.

# KMC FC yafanikiwa kumnasa Pipino

Na Somoe Ng'itu

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa KMC FC umetangaza kumsajili kiungo, Ahmed Bakari 'Pipino' kutoka Kituo cha Magnet cha jijini, Dar es Salaam.

Taarifa rasmi zilizotolewa na klabu hiyo inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni jijini, zinasema mchezaji huyo amesaini mkataba wa miaka miwili.

"Tunapenda kumtangaza rasmi Ahmed Bakari 'Pipino' ni mchezaji halali wa KMC 'KinoBoys'.

Pipino alikuwa mmoja wa wachezaji walioisaidia Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), ambayo hivi karibuni ilitwaa ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20).

Wakati huo huo, Kikosi cha KMC kiliondoka Dar es Salaam jana na kuelekea Arusha kuwafuata wenyeji Coastal Union kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini humo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, KMC yenye pointi 18 iko kwenye nafasi ya tisa huku vinara wakiwa ni Simba yenye pointi 37.

Ligi hiyo inayotoa wawakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itaendelea tena leo kwa Singida Black Stars kuwakaribisha Simba kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida.



Wachezaji wa Coastal Union ya Tanga wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC kutoka Dar es Salaam, itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha. **PICHA: MTANDAO**

# Zanzibar Heroes yaingia kambini

Na Somoe Ng'itu

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), kimeingia kambini tayari kuanza maandalizi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajiwa kufanyika hivi karibuni Kisiwani Pemba.

Mashindano ya Kombe la Mapinduzi 2025, safari hii yanashirikisha timu za taifa na wenyeji Zanzibar Heroes watakuwa chini ya Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco'.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Zanzibar Heroes, Hassan Mussa Ibrahim, alisema kikosi hicho kimeanza maandalizi mapema kwa sababu wanahitaji kufanya vyema michuano hiyo.

**Ibrahim alisema kikosi hicho kitaendelea Pemba ifikapo Januari Mosi na wanaamini wataonyesha ushindani katika michuano hiyo.**

"Tunawaomba wadau kujitokeza sasa kuisaidia timu hii. Hii ni fursa kwa kila Mzanzibar kuisaidia timu, tusisubiri kupata mafanikio, tuwakopeshe wachezaji wetu kwa kuwafanyia hisani wakati wa maandalizi," alisema mratibu huyo.

Naye Mohammed Ibrahim Raza (Raza Lee), ambaye amekabidhi vifaa vya michezo kwa Zanzibar Heroed, aliliambia gazeti hili ameamua kuipatia timu hiyo vifaa kwa sababu anaamini itakwenda kupeperusha vyema bendera ya Zanzibar.

"Huu ni wakati wa wananchi wa Zanzibar kusimama na timu yao ya taifa baada ya kukosa kuiona kwa muda mrefu," alisema Raza Lee.

Wakati huo huo, Morocco amewaondoa katika kikosi chake, Ibrahim Mkoko kutoka Namungo FC na Abdallah Said 'Laso' wa KMC, zote zinashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kutokana na utovu wa nidhamu.

Badala ya nyota hao, kocha huyo amemwita Ali Juma Maarifa (Mabata), kutoka Uhamiaji FC ya Zanzibar.

Timu nyingine zinazotarajiwa kushiriki mashindano hayo ni Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars, Burundi, Kenya, Uganda na Burkina Faso), na zote zinatumia michuano hiyo kama sehemu ya maandalizi kuelekea Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA EDERSON

MANCHESTER United inamchunguza, Ederson wa Atalanta mwenye umri wa miaka 25, na kiungo huyo wa kati wa Brazil ni mmoja wa wachezaji wachache ambao klabu hiyo inazingatia sana kuwapata. (***Florian Plettenberg***)

### FERGUSON AGEUKA LULU

WEST Ham, Leicester City na Southampton zinaongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Brighton. (***Givemesport***)

### DIBLING SAFARI IMEIVA

KLABU ya Southampton inaweza kumuuza mchezaji wao chipukizi, Tyler Dibling, mwenye umri wa miaka 18, ikiwa watashuka daraja kutoka Ligi Kuu, huku Manchester United na Newcastle United zikionyesha nia ya kumnunua kiungo huyo wa kati wa Uingereza. (***Football Insider***)

### POGBA ASAKA TIMU

UVUMI umeena kuhusiana na kiungo wa zamani wa Manchester United na Juventus, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 31, alikuwa ameonekana kwenye uwanja wa mazoezi wa Manchester City haukuwa wa kweli. (***Fabrizio Romano***)

### FAGIOLI KUONDOKA JUVE

WEST Ham, Fulham, na Crystal Palace zote zinamfuatilia kiungo wa Juventus, Nicolo Fagioli, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 23 anavutiwa na Tottenham Hotspur. (***Tuttosport***)

### SESKO ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inafikiria uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Slovenia, Benjamin Sesko, mwenye umri wa miaka 21. (***TeamTalks***)

### HJULMAND MAMBO SAFI

BOSI wa West Brom, Carlos Corberan na kocha zamani wa Denmark, Kasper Hjulmand, anatajwa huenda akachukua nafasi ya Russell Martin huko Southampton, lakini bosi wa muda, Simon Rusk, atabakia kuiongoza timu hiyo katika mechi dhidi ya Fulham hapo kesho. (***Sky Sports***)

### DUBRAVKA ANUKIA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Shabab inavutiwa na dili la bei iliyopunguzwa kwa mlinda lango wa Newcastle United na Timu ya Taifa ya Slovakia, Martin Dubravka, mwenye umri wa miaka 35. (***I***)

### DANSO SOKONI JANUARI

KLABU ya Wolves inaweza kufanya mchakato wa uhamisho wa mlinzi wa kati wa Timu ya Taifa ya Austria, Kevin Danso, mwenye umri wa miaka 26, ambaye Lens inaweza kutaka kumuuza dirisha la usajili la Januari. (***L'Equipe***)

### AKLIOUCHE AIOTA BARCA

KIUNGO mshambuliaji wa Monaco na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Maghnes Akliouche, mwenye umri wa miaka 22 amesema angependa kuichezea Barcelona katika maisha yake ya soka. (***Sport***)

### NELSON KUONDOKA ARSENAL

WINGA wa Arsenal, Reiss Nelson, ambaye anaichezea Fulham kwa mkopo ataruhusiwa kuondoka kwa Washikabunduki hao msimu ujao kutokana na uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kutokuwa sehemu ya mipango ya Mikel Arteta. (***Mail Plus***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SALAH: UBINGWA EPL MSIMU HUU NI WETU

**Mshambuliaji huyo wa Misri afikisha mabao 100 katika...**

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah amesema ana matumaini Liverpool wanaweza kunyanyua taji la Ligi Kuu England maarufu EPL msimu huu kwa sababu ni 'msimu huu' kwao ni wa kitofauti.

Kocha wa Liverpool, Arne Slot, yuko katika msimu wake wa kwanza kuinoa timu hiyo, lakini anaweza kufikia kiwango cha Jürgen Klopp kwa kupeleka taji la ligi kwa klabu hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Leicester City hapo juzi.

Salah, ambaye amekuwa akisema mara kwa mara anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu, alitoa wito kwa wachezaji wenzake wa Liverpool kuendelea kuupambania ubingwa.

**"Jambo muhimu zaidi ni timu kushinda, natumaini tutashinda Ligi Kuu," ali iambia Amazon Prime.**

"Ni nzuri, lakini tunazingatia kila mchezo na tunatumaimi tutaendelea hivyo.

"Mwaka huu ninahisi tofauti, lakini jambo la muhimu zaidi tunahitaji kutulia."

Salah alifunga bao la tatu dhidi ya Leicester, likiwa ni bao lake la 100 akiwa Anfield tangu ajiunge na klabu hiyo mwaka 2017.

"Bao zuri tena," alisema Slot kuhusu bao la 16 la Salah la Ligi Kuu msimu huu.

Kuhusu mustakabali wake Liverpool, fowadi huyo wa Timu ya Taifa ya Misri alipuuza swali kuhusu hali ya mkataba wake.

Kwa hali ilivyo, ataruhusiwa kuanzia Januari Mosi, kuzungumza na klabu nyingine kuhusu uhamisho wa bila malipo msimu wa joto.




# JORGINHO: NINA FURAHA ARSENAL

**LONDON,** England


KIUNGO wa kati wa Arsenal, Jorginho amesema furaha yake iko juu katika klabu hiyo huku wakiendelea na jitihada zao za kushinda taji lao la kwanza la Ligi ya Englad ndani ya takribani miaka 20.

Akizungumza katika mahojiano ya kipekee na ESPN Brasil, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 alisema anafurahishwa na Arsenal, ambapo amecheza mechi 66 katika mashindano yote tangu ajiunge nayo Januari, mwaka jana.

"Nina furaha nikiwa Arsenal. Huwezi kukosa furaha katika klabu kama hii, pamoja na watu wanaofanya kazi kwenye klabu, na kundi, hali ya hapa kwenye uwanja wa mazoezi. Nadhani ni mazingira mazuri ya kufanya kazi ambayo mtu yeyote anayekuja hapa anafurahia sana.

Ninaifurahia. Nimesema hapo awali siku zote nimeambiwa: 'Utakuwa kocha baadaye, utakuwa kocha.' Na kila mara nilisema: 'Hapana, sitaki, sitaki.' Kwa sababu, tupende usipende, inatokea maisha kama kocha huchukua muda zaidi, muda mwingi zaidi kuliko maisha yetu kama mchezaji, ambayo yana shughuli nyingi," alisema Jorginho.

"Kwa hiyo siku zote nilisema sitaki na nilifika Arsenal na wakasema: 'Kwa nini usifanye kozi?' Kisha nikasema: 'Oh, unajua nitafanya nini basi', ili tu, nipende au nisipende, nione jinsi ilivyo ... niliishia kupenda wazo hilo? ya kuwa uwanjani na kuweza kuwa na mchango kwa wachezaji au watoto au yeyote yule kwa hivyo ilikuwa nzuri sana na nadhani inaweza kuwa njia ya siku zijazo."



# Guardiola: City bado ni shida

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema Manchester City haitatulia kwa marekebisho ya muda mfupi katika dirisha la uhamisho la Januari.

City walitoka sare ya 1-1 na Everton kwenye Uwanja wa Etihad juzi ikiiwa ni sare ya kwanza katika michezo 13 iliyopita katika mashindano yote.

Guardiola alisema anahitaji wachezaji wapya Januari, lakini alisisitiza klabu itaangalia tu usajili ambao unaweza kuleta matokeo kwa "miaka minne au mitano."

"Dirisha la uhamisho wakati wa baridi sio rahisi," alisema Guardiola.

"Hata wachezaji wanajua tunatakiwa kuongeza wachezaji wapya, lakini baada ya wachezaji hawa kuja kucheza katika nafasi zao basi wanakosa furaha.

"Lakini tuna majeruhi wengi na hili ni tatizo. Ni kuhusu kuleta mchezaji kwa miaka minne au mitano ijayo na tutalazimika kuona. Wakati mwingine sio rahisi. Tunapaswa kujaribu."

# United mambo magumu zaidi

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim, ametoa wito kwa timu hiyo kuwa wakali zaidi baada ya kipigo cha cha mabao 2-0 kutoka kwa Wolves hapo juzi.

Matokeo hayo yameifanya Manchester United kupoteza kwa mara ya tatu mfululizo na kumaanisha timu hiyo imeshinda mechi mbili pekee kati ya nane za Ligi Kuu England.


United walipata pigo wakati nahodha, Bruno Fernandes, alipoonyesha kadi wekundu dakika mbili baada ya muda wa mapumziko kabla ya Matheus Cunha kufunga na kuipeleka Wolves mbele, huku Hwang Hee-Chan, akipachika goli pili katika dakika za mwisho za mchezo.

"Lazima tuboreshe uhusiano, lakini tuna muda kidogo," alisema Amorim akiiambia Amazon Prime baada ya mchezo.

"Tunakosa uchokozi kidogo, lakini tunacheza tu na kujaribu kutafuta njia bora ya kushinda michezo na ndivyo hivyo. Hatuwezi kudhibiti michezo kama ile tuliyopoteza. Nafikiri tulikuwa tukidhibiti mchezo kila wakati, sio tu kutawala, lakini katika udhibiti wa baadhi ya mambo."

Mapambano ya United yameendelea chini ya Amorim, ambaye alichukua nafasi ya Erik ten Hag mwezi uliopita, huku timu hiyo ikishinda mara nne pekee katika mashindano yote.

Hii ni mara ya kwanza kwa United kupoteza michezo mitatu mfululizo katika mashindano yote tangu Septemba mwaka, 2023.



## HABARI MICHEZO

### Simba, Singida BS zaidi ya fainali leo

INATOKA UKURASA 24

katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 33 kibindoni.

Baada ya mechi hiyo, Simba itarejea Dar es Salaam kuanza maandalizi ya kuelekea Tunisia kuwafuta, CS Sfaxien kwa ajili ya mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Januari 5, mwakani.

### Mzize aanika 'dawa' iliyomwokoa Dube

INATOKA UKURASA 24

inayoendelea.

"Leo hii unaona kila kitu sasa kimebaki historia na kila anachofanya kinakubali, amekuwa mwenye furaha sana," alisema Mzize.

Dube, aliyesajiliwa msimu huu akitokea Azam FC, alikuwa katika wakati mgumu, akiwa anakosa mabao mengi ya wazi katika michezo mbalimbali kiasi cha kuzua mijadala kutoka kwa mashabiki na wachambuzi wa soka.

Bao alilofunga nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo dhidi ya TP Mazembe katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kuifanya Yanga kutoka sare ya bao 1-1 ugenini, Desemba 14, mwaka huu lilikuwa kama limemfungulia milango kwa sababu baada ya hapo amekuwa akifunga mabao mfululizo.

Desemba 19,mwaka huu, alifunga hat-trick na kuiwezesha Yanga kuondoka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Mashujaa FC, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, akifunga bao moja katika kila mchezo, dhidi ya Prisons na Dodoma Jiji, Jumatano iliyopita, wakishinda mabao 4-0 kila mechi.

Kutokana na kufunga mabao katika mechi tatu mfululizo ya za ligi na kufikisha mabao matano, ameingia katika nafasi ya nne ya wafungaji wa Ligi Kuu, akiwa sawa na Edgar William wa Fountain Gate, Leonel Ateba wa Simba, Peter Lwasa wa Kagera Sugar.

Kwa sasa ndiye kinara wa mabao kwenye kikosi cha Yanga, akifuatiwa na Ibrahim Hamad 'Bacca' na Clement Mzize ambao wote wana mabao manne kila mmoja.

Mzize alisema mabao mawili aliyofunga kwenye mchezo uliopita dhidi ya Dodoma Jiji, yamemfanya awe na hamu ya kufunga mengi zaidi ili awe kinara si wa ufungaji ndani ya Yanga, ila Ligi Kuu Tanzania Bara.

# MABONDIA WAZAWA WAIBEBA TANZANIA KATIKA TKO YA MAMA

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuendeleza michezo nchini imezidi kung'aa baada ya mabondia wa wazawa kufanya vizuri katika mapambano ya 'Knockout ya Mama' yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa The Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam juzi na kufanikiwa kuibakiza mikanda yote Tanzania.

Pambano hilo limewakutanisha mabondia kutoka Ufilipino, Burundi, Afrika Kusini, Nigeria na wenyeji Tanzania likiongozwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliyemwakilisha Rais Samia.

Rais Samia alinogesha patashika hiyo kwa kutoa bonasi ya Sh. milioni 10 kwa Watanzania watakaoshinda mikanda ya ubingwa kwa Knock Out (TKO) na Sh. milioni tano kwa wale watakaoshinda kwa pointi na Sh. milioni moja kwa wale ambao walitamba kwenye mapambano ya kimataifa yasiyokuwa ya ubingwa.

"Wosia wangu mchezo vizuri, sheria zifuatwe," alisema Rais Samia alipokuwa akizungumza na mashabiki na kuwataka mabondia kuiheshimisha nchi katika nyanya za kimataifa, kupitia sekta ya mchezo wa ngumi.

"Nimesikia kuna mabondia kutoka nje ya nchi, mabondia wetu Watanzania mpewe Bendera ya Taifa na muipiganie nchi yenu," alisisitiza Rais Samia.

Naye Waziri Mkuu, Majaliwa, alieleza namna mchezo wa ngumi unavyopendwa nchini na kusema ni mchezo wa tatu kupendwa baada ya soka na kikapu.

Mtanzania aliyefungua dimba la ubingwa ni Yohana Mchanja aliyetwaa ubingwa wa World Boxing Organisation Global Championship dhidi ya Miel Farjado kutoka Ufilipino huku Salmin Kassim akimchapa, Adrian Lerassan, wa Ufilipino kwa pointi 3-0 na kutwaa ubingwa wa Mabara.

Ibrahim Mafia alitwaa taji la WBC Afrika kwa kumchapa kwa pointi, Lusizo Manzana kutoka Afrika Kusini huku Said Chino akitetea Ubingwa wa Mabara wa IBA kwa kumchapa kwa pointi, Michael Klassen raia wa Afrika Kusini na Kalolo Amir alishinda kwa pointi dhidi ya Shile Jelwana wa Afrika kusini na kutwaa wa PST.

Katika mapambano mengine yasiyokuwa ya ubingwa, Maisha Samson alichapwa kwa TKO, sekunde ya 218 ya pambano dhidi ya Mtanzania mwenzake, Juma Thabiti huku Omari Omari akikutana na kipigo kama hicho kutoka kwa Shauri Athumani katika raundi ya tano na Luqman Kimoko alimchapa Bismark Saah wa Ghana kwa pointi.

Naye Leila Macho alimchapa Agnes Mtimaukanena wa Burundi kwa pointi wakati Fadhil Majiha alimwadhibu kwa pointi za majaji wote, John Zile kutoka Ghana na Mganda Latibu Muwonge alikalishwa kwa kipigo cha TKO na Abbada Cadabra dakika ya 2:22 wakati Abdulrahman Magoma akishinda kwa pointi dhidi ya Festus Simon.

Bondia raia wa India, Gurpreet Signh alipigwa kwa TKO dakika ya 1:50 na Said Bwanga baada ya kuumia mkono wa kulia ulingoni wakati Salim Mtango (Mesi wa ngumi) akikutana na zomea zomea ya mashabiki baada ya kutangazwa mshindi kwa pointi dhidi ya Azeez Lateef wa Nigeria.




Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), wakimsikiliza Rais wa shirikisho hilo, Wallace Karia (hayuko pichani), katika mkutano mkuu wa mwaka uliofanyika Moshi mkoani, Kilimanjaro Jumamosi iliyopita. **PICHA: TFF**

# Fountain Gate yaihofia Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

TUMEKOSA muda wa kujiandaa, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Fountain Gate FC, Mohammed Muya, kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Muya alisema kikosi chake hakijapata muda wa kufanya mazoezi na kilianza safari ya kuja Dar es Salaam kikitokea Lindi, muda mfupi baada ya kumaliza mchezo dhidi ya Namungo FC.

Muya alisema wanafahamu na wako tayari kuikabili Yanga ingawa wanajua mechi hiyo itakuwa ngumu.

"Hatujapata muda wa kujiandaa na mchezo huo, isipokuwa tutapambana kadri ya uwezo wetu ili tusiwaangushe mashabiki wetu, tofauti ya muda imekuwa ni ndogo kutoka mechi iliyopita na hii tutakayocheza Jumamosi," alisema Muya.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wako katika hali nzuri na wanafahamu wanatakiwa kucheza kwa juhudi ili kuhakikisha wanafikia malengo yaliyowekwa na klabu.


"Wanaendelea vyema, kila mchezaji anafahamu vyema malengo yetu ni kumaliza msimu huu katika nafasi za juu kwenye msimamo, tutapambana na kucheza kwa tahadhari kila mchezo ulioko mbele yetu," Muya alisema.

Aliongeza ushindani umekuwa ni 'mkubwa' msimu huu kwa sababu kila timu imejipanga kufanya vizuri na hii imetokana na kusajili wachezaji wenye uwezo na walioongeza chachu ya mapambano.

"Nimewapa maelekezo wachezaji wangu wahakikishe wanafanya vizuri ingawa ni wazi muda wa maandalizi haukuwa rafiki, ninawakumbusha kila wakati kumheshimu mpinzani wetu na kuongeza umakini wanapopoteza mpira, lakini pia nimewaeleza lolote linawezekana, " Muya aliongeza.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Desemba 28, 2024

UK. 21



## Salah: Ubingwa EPL msimu huu ni wetu

# Simba SC, Singida BS zaidi ya fainali leo

### Mnyama aahidi anataka kumaliza mwaka kibabe kwa...

**Na Adam Fungamwango**

ITAKUWA ni patashika nguo kuchanika kwa wenyeji Singida Black Stars FC kuwakaribisha vinara, Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida.

Hiyo ni moja ya mechi zinazosubiriwa kwa hamu kubwa na mashabiki wa soka nchini msimu huu na kuifananisha na mchezo wenye hadhi ya fainali.

**Ushindi ndio matokeo pekee yatakayowafan ya Simba kuendelea kukaa kileleni na kula si kukuu ya Mwaka Mpya 2025 wakiwa wa naongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo.**

Kocha Mkuu, Fadlu Davids, amekiri haitakuwa mechi rahisi kutokana na ubora wa wapinzani wao.

"Tunakwenda kucheza na timu nzuri, yenye wachezaji wazuri, lakini tumejiandaa kucheza na timu hiyo ili kuendeleza rekodi yetu," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema katika mchezo huo atawakosa, Joshua Mutale, ambaye amebaki Dar es Salaam, pamoja na Valentine Nouma, ambaye amekwenda kufunga ndoa nchini kwao, Burkina Faso.

Aliongeza mchezaji wake mpya winga, Ellie Mpanzu, bado hajakuwa na uwezo wa kucheza dakika zote 90, ndiyo maana amekuwa hamchezeshi dakika nyingi.

"Najua wengi wanataka kumwona Mpanzu dakika zote 90, ni kweli hata sisi tunataka kwa sababu tunajua ana vitu vingi vya kutupa ambavyo anavyo, lakini hajacheza kwa muda mrefu, hivyo hayuko fiti kucheza kwa dakika zote, taratibu anapata utimamu wa mwili na watu watamfaidi," alisema kocha huyo.

Naye kiungo wa timu hiyo, Awesu Awesu, amesema inapokuja mechi ambayo Simba wanacheza hasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, inakuwa ngumu na haijalishi timu wanayocheza nayo.

"Ni mchezo mgumu na siyo huu tu, huwa nasema siku zote kila Simba inapocheza haijalishi na Singida Black Stars, mechi zake zinakuwa ngumu, lakini itakuwa ngumu kwa sababu ina wachezaji wenye viwango vya hali ya juu," alisema kiungo mshambuliaji huyo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alilimbia gazeti hili mechi ya leo kwao ni muhimu kwa sababu mbili, kwanza wanataka kumaliza mwaka na kuingia mpya wakiwa kileleni katika msimamo wa ligi, lakini kumaliza 2024, kwa ushindi.

"Haiwezekani tumalize mwaka kwa kufungwa, tunataka tuuage mwaka huu kwa kuwapa zawadi ya ushindi mashabiki wetu, pia tunataka kuingia mwaka 2025 kwa furaha," alisema Ahmed.

Simba itaingia uwanjani ikikumbuka iko kileleni kwa tofauti na pointi moja tu dhidi na mpinzani na bingwa mtetezi, Yanga yenye pointi 36.

Wakati huo huo, taarifa za ndani kutoka Simba zinasema, Mutale ameomba kuondoka katika kikosi hicho, akitaka kutolewa kwa mkopo kwenye klabu ambayo atakwenda kucheza bila presha na kuboresha kiwango chake.

Inaelezwa viongozi wa Simba kwa sasa wapo katika mchakato huo wa kuangalia ni wapi mchezaji huyo anaweza kupelekwa nje ya nchi.

Kaimu Kocha Mkuu wa Singida Black Stars, Ramadhani, amesema wamejiandaa kucheza kutokana na ubora wa wapinzani wao.

"Tumejiandaa kutokana na ubora wa Simba, najua watakuja na maswali mengi ya kutuuliza, na sisi pia tutawapa maswali, itakuwa mechi kubwa, nzuri, inayohitaji umakini mkubwa kwa wachezaji, timu zote mbili zina wachezaji bora wenye uwezo wa hali ya juu, hivyo itakuwa mechi bora na ya kuvutia," kocha huyo alisema.

Singida Black Stars ipo

INAENDELEA UK. 23



Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, akionyesha ufundi katika mazoezi ya timu hiyo ambayo leo itakutana na wenyeji Singida Black Stars katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani, Singida. **PICHA: MTANDAO**

## Mzize aanika 'dawa' iliyomwokoa Dube

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Clement Mzize, amesema yeye ndiye alikuwa mshauri nasaha 'mkubwa' wa mshambuliaji Mzimbabwe, Prince Dube,wakati alipokuwa akipitia kipindi kigumu cha ukame wa mabao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mzize, alisema ana urafiki wa karibu na Dube, hivyo ni mmoja wa watu ambao wamefurahi kuona mshambuliaji huyo anaanza kufunga mabao, kwa sababu alikuwa akikaa naye na kumpa ushauri wa nini cha kufanya.

Mzize anasema akiwa anapitia changamoto hiyo ya kushindwa kufunga mabao, Dube alikuwa kwenye hali ya kukata tamaa.

"Dube ni rafiki yangu mkubwa, ndiyo maana unaona siku ile dhidi ya Dodoma Jiji, alikuja kunipongeza kwa kunimwagia maji mechi ilipomalizika kwa sababu nilifunga mabao mawili, wote sisi ni mastraika, hata wakati alipokuwa anapitia wakati mgumu mimi nilikua mshauri wake, nilikuwa namwambia asikate tamaa kwa sababu vitu hivi vinatokea na mimi vimeshanitokea sana.

Unachotakiwa usikate tamaa, mechi yoyote utakayopewa wewe kuwa makini tu, naamini mabao yatakuja tu, ukiwa unawaza sana ndiyo unavyozidi kujipoteza," alisema Mzize.

Aliongeza Mzimbabwe huyo alimsikiliza na kufuata kile alichomwelekeza na anafurahi kuona 'kimezaa matunda' kwa sasa kufunga mabao na kufikisha magoli matano kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara



INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >